# Nipashe

Jumatatu Aprili 1, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579880

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13




## NEC yapuliza kipenga uchaguzi wa Arumeru

UKURASA 2

# Maalim Seif aacha ruzuku bil. 1/-

UKURASA 2



## Lissu kurejea nchini leo

UKURASA 3



UK. 2

## Neema ajira 5,000 kiwanda cha nyama


**MICHEZO** BOCCO, KAGERE VITANI SIMBA IKIITAFUTA YANGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Maalim Seif aacha CUF ruzuku bilioni 1/-

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amesema anawashukuru waliokwenda mahakamani kuzuia chama hicho kulipwa ruzuku kwa kuwa sasa kina malimbikizo ya ruzuku yanayofikia Sh. bilioni moja.

Miaka miwili iliyopita, wanachama na wabunge wa CUF waliokuwa wanamuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, walifungua kesi Mahakama Kuu wakiiomba iizuie serikali kutoa ruzuku kwa chama hicho hadi pale mgogoro wa uongozi utakapomalizika.

Tayari Maalim Seif ameshatangaza kukihama chama hicho, akijiunga na Chama cha ACT-Wazalendo kinachoongozwa na Zitto Kabwe.

Wakati Maalim Seif akitimkia ACT-Wazalendo, Prof. Lipumba mwishoni mwa wiki aliweka wazi kuwa anawashukuru waliofungua kesi kortini kuzuia ruzuku ya CUF kwa kuwa sasa kuna malimbikizo makubwa ya ruzuku kutokana na zuio hilo.

Prof. Lipumba (66), aliweka wazi kuwa kwa sasa wamerhusiwa kuitumia ruzuku hiyo iliyokuwa imezuiwa awali na Mahakama Kuu baada ya kufunguliwa kwa kesi ya kupinga kutolewa kwake.

"Tena tunawashukuru wale waliozuia ruzuku kwa sababu wamezuia ruzuku pakawa na malimbikizo, sasa yale malimbikizo yakawa yamekuwa makubwa, nadhani ilikuwa karibu (shilingi) bilioni," Prof. Lipumba alisema.

Maalim Seif na wenzake walifungua maombi namba 80 ya mwaka 2017 katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakiiomba itoe zuio kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kutoa ruzuku kwa CUF hadi pale kesi zote za chama hicho zitakapokwisha.

Ombi hilo lilikubaliwa na Jaji Wilfred Dyansobera kwa maelezo kwamba fedha hizo ambazo hutolewa na serikali, zisitolewe kwa chama hicho kwa kuwa kuna mgogoro wa kiuongozi. Maalim Seif alitangaza kuihama CUF na kujiunga na ACT-Wazalendo muda mfupi baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutoa uamuzi wa kumtambua Prof. Lipumba kuwa Mwenyekiti halali wa CUF na kuhitimisha rasmi mgogoro wa kiuongozi uliodumu kwa takriban miaka mitatu ndani ya chama hicho.

Mgogoro huo ulianza Agosti 2015, Prof. Lipumba alipoandika barua ya kujiuzulu nafasi yake ndani ya CUF akieleza kutofurahishwa na uamuzi wa vyama vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) kumpa nafasi Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, kuwania nafasi chini ya mwamvuli wa umoja huo.

Mbali na CUF, Ukawa uliundwa na vyama vingine vitatu vya siasa ambavyo ni Chadema, NLD na NCCR-Mageuzi na Prof. Lipumba alikuwa miongoni mwa wenyeviti wenza wa umoja huo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa Jukwaa la Tafakuri jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Uzinduzi huo ulidhaminiwa na Benki ya NBC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEC yapuliza kipenga uchaguzi wa Arumeru

**Na Salome Kitomari**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imetangaza uchaguzi mdogo wa Jimbo la Arumeru mkoani Arusha utakaofanyika Mei 19, mwaka huu.

Uchaguzi huo utatanguliwa na kampeni za siku 29 mfululizo kuanzia Aprili 20 hadi Mei 18, mwaka huu, kwa wagombea wa vyama mbalimbali kunadi sera zao kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Nec, Dk. Athuman Kihamia, jana, akizungumza na waandishi wa habari alisema kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 37 na 46 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, umma unataarifiwa kuwa jimbo hilo litakuwa wazi.

Alisema kuwa fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Aprili 15 hadi 19 mwaka huu.

"Tume tunavikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya tume wakati wa kipindi chote cha uchaguzi mdogo," alisema.

Alisema walipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge aliyezingatia Kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura 343 ya sheria za Tanzania, akitaarifu Tume kuwapo kwa nafasi wazi ya ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

"Kwa mujibu wa barua ya Spika nafasi hiyo imekuwa wazi kutokana na Joshua Nassari, kupoteza sifa ya kuwa mbunge baada ya kutohudhuria mikutano mitatu ya bunge bila ruhusa ya Spika," alisema Kihamia.

Machi 14, mwaka huu, Spika aliiandikia Nec kuwa mbunge huyo amepoteza sifa baada ya kushindwa kuhudhuria vikao vitatu bila taarifa.

Taarifa ya Spika ilieleza kuwa Mbunge huyo hakuhudhuria mikutano ambayo ni mkutano wa 12 wa Septemba 4 hadi 14, mwaka jana, mkutano wa 13 wa Novemba 6 hadi 16, mwaka jana na mkutano wa 14 wa Januari 29 hadi Februari 9, mwaka huu.

Baada ya uamuzi huo, Nassari alizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa alikuwa Marekani kwa ajili ya matibabu ya mkewe na aliwasiliana na Spika kwa kutumia barua pepe kumjulisha sababu za kutohudhuria vikao.

Mbunge huyo alisema alichagua kumuuguza mkewe hadi alipofanikiwa kujifungua mtoto na kwamba angekwenda mahakamani kutafuta haki yake. Machi 18, mwaka huu, Nassari alifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Dodoma kupinga uamuzi wa Spika dhidi yake na Machi 19, mwaka huu, Mahakama ilisimamisha uchaguzi mdogo hadi uamuzi utakapotolewa.

Ijumaa, mahakama hiyo iliridhia mbunge huyo kufukuzwa ubunge kutokana na utoro.

Nassari alichaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2012 kwa tiketi ya Chadema, baada ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Jeremia Sumari, kufariki Janauri 19, mwaka 2012.

# Neema ajira 5,000 kiwanda cha nyama

**Na Mwandishi Maalum**

TANZANIA na Misri zimeweka historia nyingine ya ushirikiano baada ya kutia saini hati ya makubaliano ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuchakata nyama na mazao mengine ya mifugo kinachotarajiwa kutoa ajira kwa takribani watu 5,000.

Imeelezwa kuwa kiwanda hicho kitakajengwa kwa ubia baina ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) ya Tanzania na Kampuni ya Necai ya Misri na baada ya ujenzi wake kukamilika, kitazalisha nyama na bidhaa za ngozi kama viatu, mikanda, mabegi na chakula cha mifugo.

Kiwanda hicho kitakachoitwa Ruvu Integrated Industry kikiwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,500 na mbuzi 4,500 kwa siku, kitajengwa katika Ranchi ya Ruvu wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano hayo baina ya nchi hizo jijini Dar es Salaam juzi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema ujio wa kiwanda hicho ni faraja kubwa kwa wafugaji hasa katika kipindi hiki ambacho hawana masoko ya uhakika ya mifugo yao.

Waziri Mpina alisema ujenzi wa kiwanda hicho pia kunapeleka salamu njema kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Maendeleo Mashariki mwa Afrika (IGAD) na mataifa mengine ambayo yanategemea mazao ya mifugo kutoka Tanzania.

Alisema asilimia 1.4 ya mifugo yote duniani iko Tanzania na asilimia 11 ya mifugo yote Afrika iko Tanzania, hivyo kuna uhakika wa viwanda hivyo vinavyoanzishwa sasa kupata malighafi ya kutosha muda wote.

Aliihakikishia Misri kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kufanya mageuzi makubwa katika uzalishaji wa mifugo pamoja na huduma za mifugo ili kuhakikisha malighafi hiyo ya viwanda inakuwa bora na inapatikana wakati wote.

Waziri Mpina aliagiza timu ya wataalamu kutoka Tanzania na Misri kukamilisha haraka upembuzi yakinifu wa mradi huo ili ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa, mkataba rasmi wa ubia wa ujenzi na uendeshaji wa kiwanda hicho uwe umesainiwa.

Pia aliwaagiza watendaji wote wa serikali wanaoshiriki katika majadiliano hayo kutoa ushirikiano wa kutosha katika kufanikisha mkataba huo kutiwa saini.

Watendaji wanaohusika ni wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano

INAENDELEA UK.8

HABARI KITAIFA

# Tundu Lissu kurejea nchini leo

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, anatarajiwa kutua nchini leo akitokea Ubelgiji alikokwenda kwa matibabu mwanzoni mwa mwaka jana.

Januari 6, mwaka jana, Lissu alitoka kwenye Hospitali ya Nairobi, Kenya na kwenda Ubelgiji kuendelea na awamu ya pili ya matibabu yake ya kibingwa kutokana na kushambuliwa kwa kupigwa risasi.

Taarifa zilizoifikia Nipashe jana kutoka ndani ya familia ya Mbunge huyo wa Singida Mashariki (Chadema), zilidai kuwa mtaalamu huyo wa sheria atatua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere leo saa 3:40 asubuhi kwa ndege ya KLM.

Chanzo chetu kilidai kuwa Lissu baada ya kuwasili nchini, atakuwa na mazungumzo na viongozi wakuu wa Chadema na baadaye atakwenda Dodoma kuungana na wabunge wenzake kushiriki mkutano wa Bunge la Bajeti utakaoanza kesho.

Lissu (51), alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana Septemba 7, 2017, wakati akijiandaa kushuka kutoka kwenye gari lake nyumbani kwake Area D mjini Dodoma ikiwa ni muda mfupi baada ya kuahirishwa kwa kikao cha mchana cha Bunge ambacho pia alipata nafasi ya kuchangia hoja.

Baada ya shambulio hilo, Lissu alipelekwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na kupatiwa matibabu ya awali kisha kusafirishwa kwenda Kenya kwa matibabu ya kibingwa.

Mbunge huyo aliondoka Kenya kwenda Ubelgiji akisafiri kwa ndege ya KLM iliyomchukua kutokea Amstedam, Uholanzi hadi kwenye Uwanja wa Ndege wa Zaventem alikopokewa Januari 6, 2018 saa 11:40 jioni na kupokewa chini ya ulinzi mkali wa maofisa wa polisi.

Rais huyo wa zamani wa Chama cha Wanasheria (TLS) alianza safari yake ya matibabu ya tatu akitokea Nairobi, Kenya kwa ndege ya KQ siku hiyo saa mbili asubuhi.

Imekuwa ikielezwa na baadhi ya wachambuzi wa masuala ya siasa nchini kuwa kuna uwezekano mkubwa Lissu akapeperusha bendera ya Chadema kuwania kiti cha urais wa Tanzania katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Hivi karibuni, Lissu alitoka hospitalini Ubelgiji na kufanya ziara katika baadhi ya nchi za Ulaya na Amerika na kuweka wazi kuwa kama chama chake kitaona anafaa kukiwakilisha kuwania kiti cha urais wa Tanzania mwakani, atakuwa tayari kufanya hivyo.

*Kumbuka tarehe ya leo ni siku ya wajinga.

# Mengi, MO waombwa mijadala ya kujiajiri

**Na Elizabeth Zaya**

WABUNIFU wanaochipukia wamesema upo umuhimu kwa wafanyabiashara wakubwa nchini kuanzisha mijadala mbalimbali, pamoja na kuandika vitabu vya kuwahamasisha vijana kujifunza mbinu za kujiajiri.


Kauli hiyo ilitolewa na baadhi ya vijana wabunifu katika Wiki ya Ubunifu iliyomalizika Machi 30, jijini Dar es Salaam.

Wiki hiyo iliandaliwa na Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF), kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la UKaid.

"Watanzania tulikuwa hatujajengwa katika mfumo wa kumweka mtu katika mazingira ya kujiajiri, asilimia kubwa tulikuwa tunaamini kwamba lazima tusome sana na tufaulu vizuri ili tupate kazi nzuri ya kuajiriwa, lakini kadiri siku zinavyokwenda maisha yanabadilika, teknolojia pia inakua na kutulazimisha tuendane nayo," alisema mmoja wa washiriki wa wiki ya

INAENDELEA UK. 8



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Profesa Philemon Wambura na Mwenyekiti wa Kampuni ya NECAI ya Misri, Ahmed Hassan Ahmed Mohamed, wakisaini hati ya makubaliano ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha nyama Ruvu. Wengine wanaoshuhudia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina na Balozi wa Misri, Mohamed Gaber Abulwafa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Mvua yawaacha 20,000 bila makazi

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

KAYA 76 zenye wakazi 19,883 katika Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, zimeachwa bila makazi baada ya nyumba zao kuezuliwa na mvua ya mawe iliyoambatana na upepo mkali.

Mvua hiyo pia imesababisha uharibifu wa hekari 150 za mazao mchanganyiko katika halmashauri hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama Annamlingi Macha, alisema mwishoni mwa wiki kuwa mvua hiyo imesabababisha watu 19,883 kukosa makazi na kulazimika kupata hifadhi ya muda kwa majirani ambao nyumba zao hazikuezuliwa.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa za athari za mvua hiyo, timu yake ilifika kutoa msaada wa dharura kwa watu hasa wazee ambao nyumba zao zilianguka na wakakosa mahali pa kuishi.

Macha alisema majanga yanatokea kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi, akiwataka wananchi kulinda na kutunza mazingira kwa kupanda miti kuzunguka nyumba zao na katika maeneo mengine na kuacha tabia ya ukataji miti ovyo.

Shirika lisilokuwa la kiserikali la Capacity Building Initiative for Poverty Alleviation (Cabuipa) kwa kushirikiana na Oxfarm walitoa msaada wa chakula kwa waathirika wa mvua hizo wenye thamani ya Sh. milioni 10.202. Meneja mradi wa shirika hilo, Projestus Bakenga, alisema lengo la shirika hilo ni kujenga uwezo kwa jamii ili kuondokana na umaskini.

Alisema shirika linatekeleza mradi wa kupunguza athari za maafa kwa kuimarisha ustahimilivu wa jamii zilizoathiriwa na maafa au majanga ili kukabiliana na athari hizo.

Alisema msaada walioutoa kwa waathirika wa mvua hizo ni unga wa mahindi Kg 2,660, maharage Kg 319, sukari Kg 76, unga wa lishe kwa watoto Kg 163, chumvi Kg 38 na mafuta ya kupikia lita 532.

Mbunge wa Msalala, Ezekiel Maige (CCM), alitoa pole kwa waathirika wa mvua hizo na kueleza kuwa tayari ameomba misaada kwa wadau mbalimbali likiwamo shirika.

Maige pia alimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Kahama (Macha) kwa msaada na ushirikiano anaoutoa kwa jimbo lake, akidai kuwa kwa miaka 13 ya ubunge, alikuwa hajawahi kupata ushirikiano wa aina hiyo kutoka kwa mkuu wa wilaya.

# Vyanzo ajali barabarani vyatajwa

**Na Mary Geofrey**

KATI ya ajali za barabarani 3,732 zilizotokea mwaka 2018 na kusababisha vifo vya watu 1,788 na majeruhi 3,746, miongoni mwa waliosababisha ni watembea kwa miguu 259 sawa na watu wawili kwa siku tatu walisababisha ajali moja.

Wengine ni madereva wa pikipiki 725, waliosababisha ajali kwa mwendokasi 364, madereva wazembe 1,556, walevi 61 na waendesha baiskeli 103.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alitoa takwimu hizo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua kongamano la kwanza la kitaifa la usalama barabarani lililowahusisha wadau mbalimbali wa masuala ya usafiri na maofisa wa Jeshi la Polisi nchini.

"Katika kipindi cha mwaka jana pekee jumla ya ajali 3,732 zilitokea nchi nzima ambazo zilisababisha vifo vya watu 1,788 na majeruhi 3,746 na ajali zimesababishwa na uzembe wa madereva, watembea kwa miguu, madereva pikipiki na walevi," alisema Lugola.

Aidha, alisema ajali hizo zimepungua ikilinganishwa na mwaka 2017 zilikuwa ajali 5,574 zilizosababisha vifo vya watu 2,581 na majeruhi 5,489.

Alieleza kuwa tofauti ya ajali katika miaka hiyo miwili ni kutokana na juhudi zilizofanywa na wadau wa usalama barabarani

INAENDELEA UK. 8

TUNAKUFIKIA POPOTE ULIPO TANZANIA
TANGAZA NASI SASA!!




Wawakilishi wetu wa mikoani
Iringa: Siangicha Ngowi- 0658269470
Tanga: Elisha Eliya Eliya 0719923993
Arusha: Hevens Mrema – 0754481773
Zanzibar: Marry Kizuguto- 0714262437
Dodoma, Singida: Sultan Ally -0714889096 & Raymond Mushi:0784 604262
Kilimanjaro, Manyara: Kelvin Lymo- 0715840855
Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Kigoma: Abel Manase 0715214119 & Imani Isaya 0652 751 391
Morogoro: Baragash Hassan -0659324138
Ruvuma, Lindi, Mtwara : Gideoni Mwakanosya-0754928752
Rukwa, Mbeya, Njombe: Gibson Mwakatwila 0767318070
Tabora: Halima Ikunzi- 0743868485
Shinyanga: Shaaban Njia 0757209852
Pwani: Mwombeki Mbekomize 0756756122
Dar Es Salaam: Moses Masunga 0755 642851

615126102

The Guardian
Nipashe

For More Information Please contact:
Simu: +255 767 223 311, Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
Mikocheni Light Industrial Area
SLP 31042 Dar es Salaam

# JPM ampaisha aliyekataa rushwa TRA

**Na Salome Kitomari**

ALIYEKUWA Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Kilimanjaro, Msafiri Mbibo, ameula baada ya Rais John Magufuli kumteua kuwa Naibu Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo nchini.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Gerison Msigwa, imeeleza kuwa uteuzi huo umeanza jana.

Desemba 10, mwaka huu, Rais Magufuli, akizungumza na viongozi wa TRA nchini na wakuu wa mikoa, uliofanyika jijini Dar es Salaam, aliagiza kupandishwa cheo kwa meneja huyo kutokana na kukataa rushwa ya Dola za Marekani 2,000 (sawa na Sh. milioni nne kwa viwango vya kubadilishia fedha wakati huo).

"Watu kama yule (Meneja wa Kilimanjaro) anatakiwa kupandishwa cheo, angekuwa hata mkurugenzi au nani mkubwa mkubwa, ili awasimamie wengi na kuwafundishe wengi namna ya kufanya kazi," alisema na kuongeza:

"Lakini huyo watam-frustrate (msumbua) nimesema hapa hadharani, nitafuatilia atakuwa wapi...katika nchi hii ukifanya vizuri utapigwa vita tu."

Meneja huyo alikataa rushwa hiyo kutoka kwa Meneja wa Kampuni mbili za ujenzi, Sureshbabu Kakolu, mnamo Novemba 15, mwaka jana.

Kampuni hizo ni Dott Services (TZ) Ltd na General Nile Company for Roads and Bridges/Dott Services JV.

Fedha hizo zilidaiwa kuwa ni kishawishi ili meneja huyo apitishe maombi ya msamaha wa kodi wa Sh. bilioni 6.6 ambazo kampuni hizo zililimbikiza toka mwaka 2013 hadi Oktoba 2018.

Kakolu alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Kilimanjaro, Novemba 16, mwaka jana, alihukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni moja ambayo aliilipa na kukwepa kifungo cha miaka mitatu jela.

Katika hatua nyingine, Rais amemteua Adolf Ndunguru kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango anayeshughulikia sera.

Ndunguru ameteuliwa kushika nafasi hiyo ambayo ilikuwa wazi na kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Kamishna Mkuu wa TRA.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uteuzi huo ulianza mara moja jana.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Patrick Mongella, akibadilishana nakala ya mkataba na Naibu Mkurugenzi Mkazi nchini wa SNV, Lucy Silas, baada ya kusaini randama ya ushirikiano yenye lengo la kutoa motisha kwa wadau wanaosambaza umeme wa sola vijijini, ambapo shilingi bilioni 3.8 (Euro milioni 1.5) zimetolewa kutekeleza mradi huo katika hafla iliyofanyika Makao Makuu ya TIB Dar es Salaam. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Sheria, Menson Ngahatilwa. **PICHA: MPIGA ICHA WETU**

# TIB, Uholanzi kusambaza umeme wa sola vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya TIB (TIB Development Bank) imetiliana saini mkataba wa shilingi bilioni 3.8 na Shirika la Maendeleo ili TIB isimamie utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme wa jua vijijini katika Kanda za Ziwa na Kati.

Mkataba huo umetiwa saini na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Patrick Mongella, Naibu Mkurugenzi Mkazi nchini wa SNV, Bi Lucy Fulgence Silas jijini Dar es Salaam.

Silas alisifia ushirikiano kati ya shirika lake na benki ya TIB na kufafanua kwamba mradi huu ni wa pili ambao unaanzia Kanda ya Ziwa kwa sababu utafiti kadhaa umeonyesha kwamba kuna tatizo kubwa la nishati katika kanda hiyo. Silas alisema shirika lao linashughulikia upatikanaji wa umeme vijijini na mradi huu unalenga kutoa motisha kwa wadau wa sola ili wafikishe umeme kwa wananchi ambao hawana umeme vijijini.

"Tayari tuko Kanda ya Ziwa na baadaye tutaingia Kanda ya Kati. Mpaka sasa tuna mawakala 800 wanaopeleka umeme vijijini kuharakisha maendeleo. Tulipoanza tulikuwa na msambazaji mmoja, lakini kutokana na ushirikiano mzuri na TIB mpaka sasa tuna wasambazaji 11," alieleza Silas.

Mongella alieleza kuwa huu ni mradi wa pili wa umeme wa jua na kwamba TIB imejipanga kushirikiana na wadau wa Uholanzi ili kuchochea maendeleo nchini.

Mongella alitumia nafasi hiyo kuzialika kampuni na taasisi nchini kutumia huduma za TIB na kutoa mfano wa Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) ambao amesema wamefanyakazi nao kwa mafanikio. "Tunakaribisha taasisi zije tuzungumze. Sisi tunatoa mikopo ya muda mfupi na muda marefu kwa lengo la kuharakisha maendeleo," alisema.

Meneja Mradi wa SNV, John Kundael Mlay, alisisitiza kwamba fedha itatumika kwa makini katika kuzipa motisha kampuni za sola ambazo kwa dhati zitaelekeze nguvu zao zote katika kupeleka umeme wa jua vijijini.

Shirika la SNV liko nchini toka 1963 na limejikita katika kilimo, nishati, na upatikanaji wa maji salama kwa matumizi ya nyumbani.

# Chopa yaokoa zaidi ya 200

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WATU zaidi ya 250 wakiwamo watalii, wameokolewa kwa kutumia chopa maalumu za uokozi katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja, baada ya kupata matatizo wakati wa upandaji ikiwamo homa ya mlima.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Kimataifa ya Kilimanjaro Search & Rescue (KSAR), Ivan Braun, alitoa taarifa hiyo jana, baada ya shughuli za kutoa huduma kamili ya uokoaji wa dharura kwa wapanda mlima na utalii hifadhini kutimiza umri wa mwaka mmoja sasa.

"Mimi mwenyewe nimekwenda katika shughuli za uokozi mara 22 na tumefanikiwa kuokoa watu zaidi ya 250 katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote Barani Afrika kwa kutumia helikopta kwenye urefu wa mita 4,800 katika eneo la Kambi ya Cosovo kuanzia mwezi Juni mwaka 2018 na pia tumefanya kazi hiyo bure mara 50 kuokoa wapagazi, wapishi na waongoza watalii na kuwapatia matibabu.

Zaidi alisema: "Sisi tunatoa guarantee (uhakika) ya usalama kwa watalii wanaokuja Mlima Kilimanjaro na sio tu Kilimanjaro, tunazungumzia hifadhi zote za taifa na mamlaka za hifadhi kwa ujumla. Tunazungumzia Mount Meru, Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na kadhalika."

Kwa mujibu wa Braun, huduma

INAENDELEA UK. 8

# Majambazi wacharanga mapanga mke, mume

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa ni majambazi, wamevamia nyumba ya mkazi moja wa mtaa wa Majengo wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, usiku wakiwa na silaha na kumjeruhi pamoja na mkewe.

Imeelezwa kuwa tukio hilo lilitokea Ijumaa saa 9:30 wakiwa na silaha mbalimbali zikiwamo za jadi.

Akiongea kwa tabu, mmoja wa majeruhi, Nzuki Maulidi (40), mkazi wa Majengo akiwa amelezwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama wodi namba 1, alisema majambazi hao walivamia nyumbani kwake na kumlazimisha kutoa fedha.

Nzuki alisema baada ya kumvamia, walianza kunishambulia kwa kunikatakata kwa mapanga, huku akipambana nao, kisha kumtaka awape fedha.

Alisema walimkata kichwani, na kwamba mmoja alimwendea mkewe na kumtaka atoe fedha, na baada ya kukaidi alikatwa panga sikioni na kuanza kupiga kelele.

"Majambazi hao walikuwa wanne na wengine walibakia nje, huku wakisema toa hela tutakuua," alieleza huku akionyesha sehemu za kichwa na mkono alizokatwa mapanga.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mji wa Kahama, Dk. George Masasi, alikiri kupokea majeruhi hao Nzuki Maulid na mkewe, Adelina Samuel wakiwa katika hali mbaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Kamanda Abwao alisema ni kundi ambalo linasadikiwa kuwa ni la majambazi ambao walivamia nyumba kwa Nzuki wakiwa na silaha mbalimbali ikiwamo na kumshambulia pamoja na mkewe.

Alisema Jeshi la Polisi linafanya msako mkali kuhakikisha wahalifu hao wanakamatwa na kupelekwa katika vyombo vya sheria.


Tanpack Tissues Limited

PAPER TO DISPOSE?

Recycle Paper, Reduce Pollution, Conserve Environment



Offering Secured Document Destruction & Recycling Solutions for Various Grades of Paper

Partner with us for Recycling
Contact us :

DAR ES SALAAM
Mr. Deep Parmar
82 Soldering road, Mikocheni B, Opp. Sayona
Tel (Gen): +255 22 2773901/3
(Mob): +255 712 424738

ARUSHA
Mr. Suresh Kalyani
Factory Area, Unga Road
Tel (Mob): +255 754 817400

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mashabiki Simba amkeni TP Mazembe 'wafie' Taifa

**KWA** mara nyingine tena Simba itashuka katika Uwanja wa Taifa Jumamosi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, safari hii ikiwa ni mchezo wa mkondo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo.

Kama ilivyokuwa katika mechi zilizopita za Simba kwenye uwanja huo dhidi ya Nkana FC, JS Saoura, Al Ahly na AS Vita, kwa wapenzi wa soka na Watanzania kwa ujumla hususan mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao, tunaamini Jumamosi itakuwa hivyo pia.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba mtiririko wa matokeo ya Simba kwa kutowaangusha mashabiki wake na Watanzania kwa ujumla inapokuwa nyumbani, unazidi kuhamasisha wapenda soka kwenda kuishuhudia kama si kuishangilia.

Hata hivyo, licha ya Uwanja wa Taifa kutapika watu kwenye mechi za Simba zilizopita, bado mashabiki wanaonekana kutoisaidia timu vilivyo kulingana na wingi wao.

Tunasema hivyo kutokana na namna ambavyo ushangiliaji wa mashabiki wa Simba unavyokuwa kama homa za vipindi uwanjani hapo. Mashabiki wa Simba na si wa klabu hiyo pekee bali Watanzania kwa ujumla, hushangilia pale timu inapofunga tu ama mchezaji fulani anapopiga chenga ya kuvutia. Na ikitokea timu yao imetangulia kufungwa ama kupoteza uwanjani, ndiyo kabisa hunyamaza kama wamelowekwa kwenye maji baridi.

Hakika huu si ushangiliaji wenye afya kwa timu unayoitakia ushindi ikiwa na mtaji mkubwa kwa mashabiki kama ambavyo tumeshuhudiwa katika mechi zilizopita.

Hivyo, Jumamosi tunataka kuona ushangiliaji ulioenda shule kwa mashabiki kushangilia mwanzo mwisho, huku wapinzani wao, TP Mazembe wakizomewa "buuu" kila wanapogusa mpira.

Hata kama Simba itatangulia kufungwa bao, bado mashabiki wanapaswa kushangilia mwanzo mwisho ili kuwahamasisha wachezaji wao na kuzidi kuwapoteza wapinzani.

Nipashe kama mdau namba moja wa michezo, tumekuwa tukifuatilia kwa karibu namna timu za wenzetu zinavyofaidika na mashabiki wao hususan zinapocheza uwanja wa nyumbani.

Mfano mzuri ni Al Ahly, ambayo licha ya mechi zake kutoruhusiwa kuingiza mashabiki zaidi ya 1000, lakini ushangiliaji wao wakutopumzika umekuwa na matokeo chanya kwa timu.


Kadhalika, mashabiki kama wa Liverpool ya Uingereza, ambao viti kwao huonekana kama vina miba kutokana na kusimama mwanzo mwisho, huku wakiimba wimbo wao wa "You'll Never Walk Alone" hakika unapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa Simba. Tunaimani Simba wakiimba hata wimbo wao uliozoeleka wa "Oooh Kidedea" mwanzo mwisho kwa mtaji mkubwa wa mashabiki walio nao, iwe mvua ama jua, TP Mazembe itakufa kwa mabao yakutosha Taifa.

Ikumbukwe hii ni mechi ya mtoano kwa timu itakayoibuka na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa nyumbani na ugenini na si pointi, hivyo wachezaji wa Simba wanatakiwa kucheza jihadi na wakati huo mashabiki wakiitumia vema nafasi yao ya kuwa mchezaji wa 12 uwanjani.

Hii ni mechi ya kufa ama kupona inayohitaji kupata mtaji mkubwa wa mabao nyumbani, hivyo Simba, mashabiki wake na Watanzania kwa ujumla kujitokeza kwao kwa wingi tu na kuujaza uwanja haitoshi, bali kunapaswa kwenda sambamba na kushangilia kwa dakika zote 90 bila kujali wametangulia kufungwa ama la. Tunatambua TP Mazembe ni timu kubwa na yenye uwezo mkubwa, lakini hilo haliwezi kuwa tatizo kwa Simba ambayo msimu huu inarekodi asilimia 100 ya kushinda mechi zake zote za nyumbani.

Nipashe kama wadau namba moja wa michezo nchini na kwa kutambua Simba inapeperusha bendera ya Tanzania katika michuano hiyo, tunaitakia kila la kheri katika maandalizi na kisha ushindi Jumamosi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Ligi Daraja la Kwanza hadi maafa yatokee?

Na Adam Fungamwango

**KWA** muda mrefu sasa, Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara ndiyo inayoongoza kwa malalamiko.

Ndiyo ligi inayoongoza kwa kuripotiwa fujo, kupanga matokeo na mambo mengine mengi ambayo si ya kiungwana kwenye mpira wa miguu duniani, yaani 'fair play'.

Lakini kwa miaka kadhaa sasa, japo uongozi wa juu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), umebadilika lakini inaonekana hakuna juhudi zozote ambazo zinachukuliwa kuonyesha kama vitendo hivyo vinaweza kukomeshwa.

Majuzi tu, tayari tumesikia timu ya Arusha United imetangaza rasmi kujitoa kushiriki katika ligi hiyo kwa madai ya kuchoshwa na vitendo ambavyo si vya kimichezo, huku ikidai TFF kupitia Bodi ya Ligi imeshindwa kuchukua hatua stahiki kwa wanaowatuhumu.

Mkurugenzi Mtendaji wa timu hiyo, Otte Beda Ndaweka, amesema licha ya timu hiyo kuwa katika nafasi nzuri katika Kundi B, imeona si busara kuendelea na ligi hiyo kufuatia matukio mbalimbali ikiwamo kufanyiwa vurugu wakati ikicheza na timu kadhaa tangu timu ianze kushiriki ligi hiyo msimu wa 2018-2019.

Timu hiyo imejitoa ikiwa imeshacheza michezo 17, kukusanya jumla ya pointi 28, huku ikishika nafasi ya tano ambapo timu ya Geita Gold FC ikiongoza ligi hiyo ikiwa na point 33.

Bodi ya Ligi ikajibu kuwa itakachofanya ni kupitia kanuni za ligi, na itaihukumu Arusha United kupitia kanuni hizo.

Ni kweli, hata Arusha United yenyewe ilikuwa inajua kuwa itahukumiwa baada ya kujitoa, lakini Bodi ya Ligi ina kipi ilichojifunza kutokana na hatua ya timu hiyo kujitoa?

Kinachotakiwa hapa ni kwamba Bodi ya Ligi inapaswa kukaa chini na kutafakari kwa kina kuhusu jambo

**Timu hiyo imejitoa ikiwa imeshacheza michezo 17, kukusanya jumla ya pointi 28, huku ikishika nafasi ya tano ambapo timu ya Geita Gold FC ikiongoza ligi hiyo ikiwa na point 33.**

hili lililotokea. Si jambo la kawaida na la kukaa kimya kuona kuna timu imejitoa, halafu kama Bodi kuchukulia poa.

Ligi Daraja la Kwanza karibu kila msimu imekuwa ikipatwa na 'skendo' mbalimbali, ikiwamo tuhuma za upangaji matokeo, uchezeshaji mbovu kwa ajili ya kuzibeba baadhi ya timu, vurugu na ukiukwaji wa sheria na taratibu.

Kama itakumbukwa misimu mitatu iliyopita kulikuwa na skendo maarufu ya Geita Gold, Polisi Tabora, JKT Kanembwa ambayo ilifika hadi mahakamani na mwishowe ikapandishwa timu ya Mbao FC.

Wala bodi isikae kuona kuwa Ligi Daraja la Kwanza iko sawa, badala yake ilipaswa iangalie kwa jicho la tatu kwa sababu ndiyo inayopandisha timu kwenye Ligi Kuu.

Ndiyo maana tunaona kuna timu zinakuwa wababe zinapokuwa huko, lakini zikiingia Ligi Kuu zinakuwa nyanya na kusababisha ligi kukosa ushindani wa kweli.

Angalia timu ya Mbao FC, ambayo haikupaswa kupanda Ligi Kuu, lakini zilipoondolewa timu ambazo zilionekana zimepanga matokeo na kupandishwa timu hiyo imekuwa ikileta upinzani mkubwa, hivyo wengi kuona kuwa timu hiyo ndiyo ilistahili kupanda, lakini ilikuwa ikiminywa na timu ambazo zilikuwa zimeandaliwa au kujiandaa kupanda Ligi Kuu kwa mizengwe.

Kwa hili la Arusha United, Bodi ya Ligi iliangalie mara mbili mbili kwa sababu huko mbele inaonekana kuna viashiria vya uvunjifu wa amani, na asisubiri hadi maafa yatokee ndiyo ianze kuchukua hatua. Ni lazima ihakikishe kuwa mechi zote zinachezwa kwa haki na mshindi anapatikana kwa juhudi zake za soka la uwanjani.

## MJADALA/BARUA

# *Tujipange na mvua hizi*

**Mhariri,**

*NAANDIKA barua hii kwanza kuwapongeza ndugu na jamaa waliokusanyika kufanya maombi katika baadhi ya sehemu, wakitaka mvua zinyeshe nchini, kutokana na jua kali ambalo linakausha ardhi na mimea. Ni hali isiyo ya kawaida.*

*Sasa kuna dalili kwamba, mvua zinataka kunyesha na kuna baadhi ya maendeleo kama wenzetu wa Dar es Salaam na mkoa Pwani. Katika lugha ya matumizi ya simu ni kwamba mvua 'imebipu' kwao na wameshaanza kuiona dalili njema.*

*Kwa ujumla wetu jamii ya wakulima, hii ina ishara kubwa sana kwetu katika mustakabali wa kilimo kwa jumla.*

*Shughuli za kupanda zimefika mahali pake. Ni namna gani wakulima tumejiandaa, kwa maana ya kuwa na nyenzo zote muhimu kwa upandaji kuanzia na mbegu?*

*Nikisema wakulima kuwa tayari, ni ujumbe ninaosafirisha moja kwa moja hadi katika uongozi wa wilaya, kwa kuwa sura na mkakati wote wa uchumi wa halmashauri iliyoko wilayani inashikiliwa na mkakati wa kiuchumi ulioko mahali hapo.*

*Binafsi nikiwa mzalishaji shambani mwenye taaluma ya darasani kuhusu kilimo, kikubwa kinachonishika wakati wote ni kwamba mafanikio ya kilimo ni tunda la pande mbili, mkulima na msimamizi wao ambaye ni serikali.*

*Inawezekana mamlaka nyingine kando yao, kama vile taasisi zisizo za serikali zinazohusika na ukuzaji kilimo nchini nazo ziko sambamba nayo kulingana na eneo hilo.*

*Ushauri wangu ni kwamba, huu ni wakati sahihi kwa halmashauri zetu katika maeneo yote kwenye umma, wadau wa kilimo, kuchukua hatua zinazostahili kuhakikisha kuja kwa mvua hizi kunachukuliwa hatua stahiki, kilimo chetu kisitetereke.*

*Kwa maana pana, tunapofanikiwa mahali hapo, hata uchumi wa taifa letu unakuwa katika mstari sahihi na unaofaa.*

**Halfan Sambika,**
**Kingolwira, Morogoro.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Watanzania tuache kumgeuza Amunike katapila Afcon 2019

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya miaka 40, Tanzania imefanikiwa kutinga fainali za Mataifa Afrika (Afcon).

Imefanikiwa kufanya hivyo baada ya kuichapa Uganda mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Taifa mwishoni mwa wiki iliyopita na kuzusha shamrashamra kwa viongozi wakuu wa nchi, pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Kwa vijana wa miaka 39, hii ni mara ya kwanza kuishuhudia Tanzania ikifuzu Afcon, kwa mara ya mwisho ilifuzu mwaka 1979 na kushiriki fainali zake mwaka 1980 nchini Nigeria, lakini sasa mwaka huu wameshuhudia kwa macho yao historia ambayo haitofutika kamwe kwenye kumbukumbu ya vitabu vya soka nchini. Lakini pia vizazi ambavyo vinashuhudia kwa mara ya pili Tanzania ikifuzu.

Baada ya sherehe hizo kupungua, kila mmoja sasa kurejea kwenye shughuli zake za kawaida, kama kawaida baadhi ya Wabongo hawaishi maneno.

Tayari kuna maneno ya chini chini ambayo yameanza kusambaa kuwa Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Emmanuel Amunike, aondolewe kwenye timu na badala yake atafutwe kocha mwingine mwenye uwezo wa hali ya juu na wasifu (CV) mkubwa kuliko yeye.

Wanadai kuwa alipoifikisha Stars panatosha na sasa hatoshi kuwa kocha mkuu wa kuiongoza Stars kwenye fainali hizo.

Wengine wanakwenda mbali zaidi na kudai kuwa kilichosababisha Stars ifuzu ni hamasa ya Watanzania, lakini pia juhudi binafsi za wachezaji. Maneno haya yalisambaa sana na kuwa mijadala kwenye mitandao ya kijamiii na wapo waliokuwa wakiunga mkono, lakini baadhi wengine wakipinga.

Mjadala ukawa mkubwa sana, kuna baadhi ya watangazaji na wachambuzi wa masuala ya michezo wakaichukua na kuihamishia kwenye vipindi vya michezo.

Huko nako Watanzania walikuwa wakitoa maoni yao. Lakini cha kushangaza wapo vile vile waliokuwa wakitaka Amunike atimuliwe kwenye kikosi cha Taifa Stars aletwe mwingine. Sababu ni zile zile, kiasi kwamba inaonekana kama vile wamekaririshwa.

Kabla ya kumuondoa Stars Amunike, kwanza Wabongo tuanze kujiuliza ni kitu gani tunachokihitaji?

Miaka 40 sasa imepita tangu Stars ifuzu, makocha wangapi wamepita kuifundisha timu hiyo na hamasa kuwapo kubwa tu?

Je, hakuna makocha ambao waliopita walikuwa maarufu na CV kubwa kuliko Amunike? Mbona Stars haikufuzu?

Sisemi kama Amunike akae milele Stars baada ya kuipeleka Afcon, lakini kwa sasa kosa lake liko wapi mpaka anaonekana hafai tena kuifundisha kutokana na mahali ambapo imefikia?

Ina maana anataka kufanywa kama katapila ambalo linatengeneza barabara na ikishamalizika, linawekwa pembeni na halifai kutumia barabara iliyotengeneza kwa sababu litabomoa?

Wale wanaosema ilikuwa ni juhudi za wachezaji, ina maana wachezaji wote wa Stars waliopita miaka yote hiyo hawakuwa na juhudi?

Wanaosema kuwa tumekwenda Afcon kwa sababu ya hamasa ya Watanzania, je, hatukumbuki kuwa Wabongo tulikuwa na hamasa kubwa miaka ya nyuma na tukajazana kwenye Uwanja wa Taifa, lakini tukafungwa bao 1-0 dhidi ya Msumbiji mwaka 2007 tukashindwa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika zilizofanyika mwaka 2008 nchini Ghana?

Hii ina maana hata kama kukiwa na hamasa, lakini kama timu haiko vizuri na kama benchi la ufundi haliko sawa ni ngumu kupata ushindi. Benchi la ufundi, maandalizi, wachezaji bora na hamasa kwa mashabiki vyote hivyo vinategemeana na vinatakiwa kwenda kwa pamoja ili mafanikio yapatikane.

Tusijidanganye Wabongo, mafanikio haya yalipatikana, pamoja na mambo mengine, lakini hatuwezi kumkwepa kocha Amunike kuwa naye amechangia, hivyo apewe heshima yake.

Nahisi kuwa Amunike amepata wapinzani wengi Bongo baada ya kuwapiga chini baadhi ya wachezaji wa Simba walipochelewa kuingia kambini siku zake za awali tu za kazi hiyo, lakini pia kutomwita Ibrahim Ajibu wa Yanga kwenye kikosi chake.

Msimamo wake wa kuamini kile anachokiamini na kutoongozwa na mawazo na mihemko ya mashabiki, ndiyo waliyosababisha baadhi ya watu kutompenda binafsi na si sababu nyingine yoyote. Kwa hiyo hata angeiwezesha Stars kwenda Kombe la Dunia, bado baadhi ya watu watakuwa na kinyongo naye.

Cha kufurahisha ni kwamba hata yeye mwenyewe anajua hilo na halipi nafasi na ndiyo maana amefika hapo alipofika.

Pamoja na kuwasifu Wabongo kwa mshikamano walioonyesha hadi kufuzu Afcon, lakini nashangaa baadhi ambao bado wana wasiwasi na kilichofanyika na kutokuwa na imani na Amunike.

Amunike ndiye kocha aliyeingia kwenye historia ya kutupeleka Afcon 2019, bado baadhi ya Wabongo tunataka aondolewe aletwe mwingine. Ili iwe nini? Kwani tulikuwa tunahitaji nini? Hivi kweli Wabongo wanajua wanachokitaka?



# Transfoma iliyoungua Mlandizi ina miaka 38

**Na Beatrice Moses**

TRANSFOMA iliyoungua na kuzua tafrani katika kituo kidogo cha kupozea umeme cha Kanda ya Mlandizi Kibaha, Mkoa wa Pwani ilitengenezwa miaka 38 iliyopita na ilikuwa na ukubwa wa MVA30 na megawati 24.

Kuungua kwa transfoma hiyo juzi, kulisababisha wakazi wa maeneo ya Mlandizi na Bagamoyo kukosa huduma hiyo kutwa nzima.

Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) limetangaza kuwa tayari limefanikiwa kurejesha huduma ya umeme kwa wakazi wa maeneo hayo, baada ya kuzuka kwa moto mkubwa.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Msemaji wa Tanesco, Leila Muhaji, alisema transfoma hiyo imetengenezwa mwaka 1981 na ilifungwa mwaka 1983.

Alisema kwa sasa thamani ya trasfoma hiyo haijajulikana na kwambaTanesco wamefanikiwa kurejesha huduma hizo kupitia wataalamu wao ambao wamemudu kuunganisha wateja hao kwenye njia nyingine.

"Kutokana na moto huo transfoma iliyoungua bado haijapatikana mbadala wake, ila mafundi wametafuta njia nyingine na kuwaunganisha ili wateja wapate huduma yetu, huku juhudi nyingine zikiendelea kufanywa," alisema Muhaji.

"Tutakapotoa tathmini ya tukio zima basi pia wataalamu watatoa thamani kwa sasa tunahakikisha wateja wanapata huduma kwa haraka iwezekanavyo na shughuli nyingine zisisimame," alisema Muhaji.

Alisema hadi sasa chanzo cha moto huo bado hakijafahamika na mafundi, wataalamu wengine wapo eneo la tukio wakidadisi sababu za moto huo.

Katika taarifa ya awali ya maandishi iliyotolewa na shirika hilo ilibainisha kuwa huduma hiyo imerejeshwa jana saa 4.51 usiku.

Awali tukio hilo lilisababisha hofu kwa wananchi walio jirani na eneo la mtambo huo ulipo jirani na mashine za maji Mlandizi kushika moto.



Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TBL, Amanda Walter, akieleza mikakati ya kampeni za usalama barabarani zinazofanywa na kampuni hiyo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola wakati wa kongamano la kitaifa la usalama barabarani lililofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni, (wa pili kulia) Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania na Katibu wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani Tanzania, SACP Fortunatus Muslimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vyanzo ajali barabarani

INATOKA UK. 4

ni ajali 1,842, vifo 793 na majeruhi 1,743.

Waziri Lugola alieleza zaidi kuwa, asilimia 76 ya ajali za barabarani zinazotokea nchini hutokana na makosa ya kibinadamu na kati ya hizo asilimia 40 hutokana na uzembe wa madereva.

Pia Lugola aliahidi kuwashughulikia maofisa na askari wa usalama barabarani wanaoendelea kujihusisha na vitendo vya kupokea rushwa.

Alisema tayari amepokea ripoti ya maofisa wanaopokea rushwa kutoka kwa kamati maalum aliyoiunda ya kuchunguza vitendo hivyo na wakati wowote kuanzia sasa atawachukulia hatua za kisheria.

Aidha, Waziri Lugola aliliagiza Baraza la Usalama Barabarani kusimamia ukaguzi wa magari ili kuhakikisha magari mabovu yanaondolewa barabarani na kupunguza ajali nchini.

Naye Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hamad Masauni, alisema mwaka huu hawajafanya maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani na badala yake wamefanya kongamano la kukutanisha wadau wote ambao walijadiliana kuhusu namna ya kuboresha utendaji kazi.

Naye Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslimu alisema operesheni mbalimbali ikiwamo ya nyakuanyakua zimesaidia kupunguza ajali za barabarani kwa kiasi kikubwa.

## Mengi, MO waombwa mijadala ya kujiajiri

INATOKA UK. 3

ubunifu, Lulu Mwagi.

Aliongeza: "Lakini historia inaonyesha kuwa wanaojiajiri ndio wanafanya vizuri zaidi na maisha yao pia yako vizuri. Kuna umuhimu wa watu waliofanikiwa kama kina Dk. Reginald Mengi (Mwenyekiti Mtendaji wa IPP), Mohammed Dewji (MO) kuanzisha mijadala ya kuelezea namna walivyofanikiwa ili kuwahamasisha vijana ambao wanaona bila kuajiriwa hawawezi kufanikiwa."

Lulu alisema hivi sasa Tanzania imejikita katika kujenga uchumi wake kupitia viwanda, hivyo kuna haja ya vijana kuchangamkia fursa hiyo kwa kubuni teknolojia mbalimbali ambazo zitatumika katika viwanda.

"Na jambo la kushukuru ni kwamba serikali imesema ipo tayari kuwashika mkono wabunifu wanaobuni vitu ambavyo vinaweza kutumika, kwa hiyo tunatakiwa tuchangamkie fursa hii, tusipende kulalamika tu," alisema Lulu.

Kiongozi Mkuu wa HDIF, David McGinty, alisema wiki hiyo ya ubunifu ambayo ni mara ya tano kufanyika imekuwa na mwitikio mkubwa kuliko iliyokuwa katika miaka mingine.

## Neema ajira 5,000 kiwanda cha nyama

INATOKA UK. 2

wa Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi nyingine zitakazohusika na mchakato wa upembuzi yakinifu.

Mbali na hilo, Waziri Mpina pia aliiomba Serikali ya Misri kuendelea kuwekeza katika maeneo mengine ya mifugo na uvuvi kwa kuwa fursa bado ni nyingi hasa katika uendeshaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (Tafico) ambalo serikali tayari imeshalifufua.

Waziri huyo alisema fursa za uvuvi wa ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) ni kubwa kwa Tanzania kwa kuwa ina eneo la kilomita za mraba 223,000, ukanda huo ukiwa unafaa kwa uvuvi wa samaki aina ya jodari na wengine ambao ni wa daraja la kwanza duniani.

Aliiomba Misri kuwekeza katika viwanda vya kuchakata samaki wa bahari na maji baridi, ufugaji wa samaki pamoja na kununua meli kubwa za uvuvi zitazovua katika maji ya ukanda wa uchumi wa bahari kuu.

Balozi wa Misri, Mohamed Gaber Abulwafa, alisema hatua ya utiaji saini hati ya makubaliano hayo ni kielelezo cha ushirikiano uliodumu kwa zaidi ya miaka 50 baina ya Misri na Tanzania katika kuchochea uchumi wa mataifa hayo mawili.

Alisema Misri imevutika kuwekeza kwenye sekta hiyo ya mifugo baada ya kubaini Tanzania inayo mifugo mingi na bora na ujio wa mradi huo ni matokeo ya mazungumzo ya awali baina ya Rais John Magufuli na Rais wa Misri, Abdel Fattah El-Sisi, alipotembelea nchini mwaka 2017.

## Chopa yaokoa zaidi ya 200

INATOKA UK. 5

ambayo wao wanatoa nchini Tanzania inaongeza chachu ya ubora kwa huduma za utalii kwa maana ya kwamba kila siku wamejiweka tayari ndani ya dakika tano pale mtu anapohitaji huduma za uokozi kwa njia ya chopa.

Kutokana na juhudi hizo za kuokoa maisha ya watu na kuongeza usalama wa watalii, Shirila la Kimataifa la World HRD Congress & Stars of the Industry Group lenye makazi yake nchini Muritus, limeitunuku tuzo nne kampuni hiyo ya KSAR iliyopo nchini Tanzania.

Tuzo hizo za mwaka 2018, ni pamoja na CEO of the Year (Ofisa Mtendaji Mkuu bora wa mwaka katika Bara la Afrika), Young Hr of the year (Ofisa Rasilimali Watu bora kwa upande wa Chipukizi wa mwaka) na Best Employer (Mwajiri bora wa mwaka Afrika) na tuzo ya mwajiri bora iliyotolewa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Pamoja na kufanikiwa kuokoa idadi hiyo ya watu, mwekezaji huyo ameeleza kufurahishwa na ushirikiano anaoendelea kuupata kutoka katika mamlaka za serikali ikiwamo Wizara ya Maliasili na Utalii, Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa), Hifadhi ya Taifa ya Arusha (Anapa), Serikali Mkoa wa Kilimanjaro na mamlaka nyingine za hifadhi, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Kampuni hiyo ya KSAR, inatoa pamoja na mambo mengine huduma kwa waliookolewa kupitia Hospitali Teule ya St. Joseph ya Moshi na kuanzisha kliniki ya kwanza maalumu Afrika kwa ajili ya matibabu ya magonjwa yatokanayo na mlima.

Kilimanjaro SAR imewekeza zaidi ya Dola za Marekani milioni tatu kwa ajili ya kuanzisha kliniki hiyo ya tiba Afrika itakayosaidia watalii wanaopata ajali na kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika hifadhi hizo.

# Huduma za bima AAR zatanua wigo

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Bima ya Afya ya AAR, imezindua huduma mpya ya bima za jumla kwa ajili ya kupanua wigo wa huduma zake.

Huduma hiyo ilizinduliwa mwishoni mwa wiki katika mkutano wake na mawakala wa bima jijini Dar es Salaam.

Kampuni hiyo ya Bima iliyokuwa ikijihusisha na bima ya afya pekee kwa miaka mingi, imeamua kuzindua sera mpya inayotanua wigo wa huduma zake za bima ili kutoa aina nyingine za bima zinazohusu ulinzi wa mali za mteja dhidi ya majanga.

Meneja Mauzo na Masoko wa AAR, Violet Tabia Massudi, alisema sera hiyo mpya iliyohuisha utoaji wa bima za jumla itaiwezesha kampuni hiyo kutoa huduma za bima mbalimbali ikiwamo bima dhidi ya majanga ya moto, ajali, magari na mambo mengine kwa lengo la kutoa fidia kwa wateja dhidi ya hasara itokanayo na majanga yasiyotarajiwa au kuonekana kabla.

Alisema kama ilivyo kwa huduma ya bima ya afya, huduma ya bima za jumla itakuwa kwenye mfumo wa 'premium'.

"Tumekuwa tukitoa huduma ya bima ya afya pekee kwa jamii na tumepata mafanikio kwa kiasi kikubwa sana na wateja wetu wamekuwa wakiridhishwa na huduma zetu, hivyo tumeamua kutanua huduma zetu bora zenye gharama nafuu ili kutoa bima za aina nyingine za jumla," alisema Massudi.

"Sera hii tuliyoizindua ni moja kati ya sera nzuri na rahisi kuelewa itayowafaidisha zaidi wateja hasa katika kupata fidia kwa wakati. Sera hii inatoa bima ya kulinda mali za watu binafsi pamoja na kampuni kwa gharama ambazo Watanzania wanaweza kuzimudu," aliongeza.

Akizungumzia sababu kuu za kutanua utoaji wa huduma zake za bima kupitia sera ya huduma za jumla, alisema wamehamasishwa na mahitaji pamoja na maombi ya wateja wao, kukua kwa uwezo wa ndani pamoja na nia ya kutaka kuihudumia jamii katika wigo mpana zaidi.

Rais wa Umoja wa Mawakala wa Bima nchini, Amir Kiwanda ambaye alihudhuria uzinduzi huo, alisema anaiona hatua hiyo ya AAR kama fursa kwa jamii kulinda mali zao kupitia kampuni ya bima inayoaminika zaidi kwa kuzingatia uzoefu wake ilipokuwa ikitoa huduma za afya pekee.

# Waliovamia makaburi waamriwa kuondoka

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WAKAZI waliovamia eneo la makaburi katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, wameamuriwa kuondoka, huku wao wakilalamika kuwa ni eneo lao halali.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo la Kyebitembe katika manispaa hiyo, wameulalamikia uongozi wa manispaa kuruhusu kufanyika kwa mazishi ya watu katika viwanja vyao karibu na nyumba wanazoishi.

Wakazi hao wamedai kwamba wanapata wakati mgumu kuishi na maiti.

Mwinjilisti Christon Christopher, alisema kuwa mwaka 2013 uongozi wa manispaa hiyo ulifika katika eneo hilo na kudai wananchi wameingilia maeneo ya makaburi na kuwataka wasiendelee kujenga hadi muafaka utakapopatikana. Alisema cha kushangaza ni kuona watu wanafika katika maeneo yao na kuzika.

"Hili ni eneo langu ambalo nimelimiliki kwa kipindi kirefu, na wakati manispaa wanapanga kuleta makaburi hapa, sisi tulishajenga na kuanza kuishi hapa," alisema. Leonidas Kajuna, alisema walikubali kufuata masharti waliyopewa kuwa wasifanye maendelezo yoyote katika eneo hilo ili kusubiri uamuzi utakaotolewa, huku akiwa na hofu kama wanaokwenda kuzika katika maeneo hayo wana vibali vya manispaa au la.

Mkuu wa Idara ya Ardhi ambaye pia ni Ofisa Mipango Miji wa Manispaa ya Bukoba, Katres Rwegasira, alisema eneo hilo liliidhinishwa mwaka 1996 na wakati huo halikuwa na makazi ya watu.

Alisema maeneo ambayo wameweka makaburi yalikuwa ni maeneo ya umma na kuwa ndiyo maana lilitengwa moja kwa moja kuwa maeneo ya makaburi.

"Hakuna nyumba wala mwananchi aliyekuwapo mwaka 1996, na tangu mchoro huo umeidhinishwa, tunategemea mtu anayekwenda kujenga pale lazima awe na kibali cha ujenzi kutoka ofisi ya mkurugenzi," alisema.

Alisema mwaka 2002/2003 ulifanyika upimaji ambao ndiyo uliweka mipaka rasmi na kupanga matumizi, na maeneo mengi ambayo hayana usimamizi wa moja kwa moja watu wanapenda kuyaingilia. "Mwaka 2012 tulikuta nyumba kama tatu na tukaweka alama ya X kwamba waondoke, lakini tukawatahadharisha wananchi kwamba wasiendelee kujenga katika maeneo haya, na ndipo eneo hili likaanza kutumika, kwa hiyo tulitoa ilani ili watu waondoke na kuruhusu wananchi kuanza kuzika," alisema.

Alifafanua kuwa waliona kuliko kuondoa watu hao kwa nguvu, bora waendelee kuzika ili wakiona makaburi yanawasonga wataondoka, lakini cha ajabu hawahami, na wengine wanazidi kuingia kujenga, kwa hiyo wote hao ni wavamizi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Limbe Moris, alisema wananchi waliojenga katika eneo hilo waondoke maana ni wavamizi. "Ninachosema wale wanaozika waendelee kuzika tu, hakuna mtu wa kuwazuia, kwa sababu hawa wamevamia, wasipotoka kwa hiari yao sisi (Manispaa) tutawatoa," alisema mkurugenzi huyo.



Baadhi ya mawakala wa bima wakisikiliza mawasilisho kuhusu bima mpya ya General Insurance, iliyozinduliwa na kampuni ya AAR jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yapewa tano kwa huduma korti kuu Kigoma

**Na Magreth Magosso,**
KIGOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Katiba na Sheria, imeipongeza serikali kwa kuwaondolea wananchi wa Kigoma adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya sheria katika Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, baada ya kurasimishwa kwa huduma ya Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma. Makamo Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Giga, alisema hawanabudi kuipongeza serikali, kwa kuwaondolea wananchi gharama za usafiri kufuata haki zao na mwendo mrefu zaidi ya kilomita 400.

"Mradi wa ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Kigoma ni kielelezo cha serikali inatekeleza dhima ya kutatua kero za wananchi hasa wenye kipato duni...kitendo cha kufuatilia mashauri yao Mkoa wa Tabora kulikuwa na upotevu wa haki," alisema na kuongeza:

"Leo huduma ipo Kigoma, ni fursa wananchi kutetea haki zao kisheria, naskia watu wa Kigoma wanajua haki zao kwa kina," alieleza Giga.

Mjumbe wa kamati hiyo, Asha Mshua, alisema lengo la kamati hiyo ni kufuatilia na kusimamia maendeleo ya miradi ya mahakama na kwa ujenzi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu ya Kigoma ni chachu ya wataalamu wa sheria kutoa haki kwa sababu jengo lina miundombinu ya kisasa itakayowapa hamasa kutoa hukumu kwa wakati na sahihi kwa shauri husika.

Wakili msomi wa kujitegemea, Daniel Rumenyela, alikiri awali walisafiri kilomita 429 sambamba na gharama kubwa kufuatilia shauri la mteja tangu mwaka 1961, lakini kuwapo kwa mahakama hiyo na jengo la kidigitali ni faida ya wataalamu kutumia vifaa vya kielektroniki kuchukua maelezo ya shauri husika, huku akipongeza serikali kwenye mradi huo.

# Malipo NEMC sasa kwa mtandao

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), limetangaza kwamba malipo yote kwa baraza hilo yatapitia mfumo wa serikali wa malipo kwa njia ya kielektroniki (GePG ). Akitangaza uamuzi huo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa NEMC, Charles Wangwe, alisema mfumo huo utarahisisha ukusanyaji wa ada na tozo mbalimbali na kuongeza kwamba mfumo huo utaondoa upoteaji wa fedha inayopaswa kulipwa kwa NEMC.

"Mfumo huu umeanza rasmi kutumika Machi 23, 2019 na utasaidia kuwaondolea kero wananchi na wadau wa mazingira katika kufanya malipo na kupelekea baraza kupata mapato stahiki kwa wakati," amesema Wangwe.

Alifafanua kuwa kumekuwapo na ucheleweshaji wa malipo ya tozo na ada za mwaka kwa wadau wa mazingira. Lakini mfumo huu utasaidia kupata taarifa kamili za malipo kwa wadau wote na kurahisisha ufuatiliaji kwa wale ambao hawajafanya malipo.

"Natoa wito kwa wananchi na wadau wa mazingira kufanya malipo ya mwaka kwa kipindi kilichowekwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Kufanya kinyume na hivyo sheria kali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kupigwa faini na kufutiwa usajili. Watakofutiwa usajili itabidi waombe upya," amefafanua.

Wangwe alifafanua kuwa watakaofutiwa usajili ni pamoja na wadau wa tathmini ya athari kwa mazingira kwa kitendo cha kutolipa tozo ya mwaka kwa wakati. Nao itawalazimu kuomba usajili upya.

"Ili kuepuka usumbufu huo ninawaomba wadau wote kutekeleza wajibu wao kwa kulipa ada na tozo stahiki kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi," alisema Wangwe. Alisema walipaji wapate 'control number' kabla ya kufanya malipo ili waweze kuepuka usumbufu kwa kuwa utaratibu mpya unahitaji namba hiyo itakayotoa utambulisho wa malipo katika huduma iliyoombwa na si vinginevyo.

"Mfumo huu utasaidia kupunguza upotevu wa fedha ambazo zilikuwa hazifiki katika sehemu husika kutokana na kupita katika mikono ya watu wengi, hivyo kupitia mfumo huu utakwenda kuondoa tatizo hilo," alisema Wangwe.



Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa NEMC, Charles Wangwe, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu utaratibu mpya wa malipo kupitia mfumo wa serikali kwa njia ya kielektroniki (GePG) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa majitaka kuleta neema ajira

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KAIMU Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga Mjini (SHUWASA), Flaviana Kifizi, amebainisha kuwa mradi wa majitaka ambao unatarajiwa kujengwa mjini hapa na wafadhili kutoka Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), utasaidia kwa kiwango kikubwa kutoa ajira kwa vijana.

Alisema mamlaka haina mfumo wa majitaka, na kwenye mradi huo ambao ndio wahusika wakuu wa kuutumia ili kuuweka mji wa Shinyanga katika madhari ya usafi wa mazingira, na kwamba itawabidi watoe ajira mpya kwa vijana ambao watakuwa wakifanya kazi kwenye eneo hilo.

Kifizi alibainisha hayo kwenye uzinduzi wa kuanza utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo, ambao utakamilika mwaka 2022 kwa kujenga pia bwawa la kuhifadhia majitaka na kuyatibu ili yasileta athari kwa wananchi na kusababisha kutokea magonjwa ya mlipuko.

"Kutokana na mamlaka yetu kutokuwa na mfumo wa majitaka, itatulazimu sasa tuajiri vijana wapya ambao watakuwa wamesomea mfumo huu, wakiwamo wataalamu wa kuyatibu majitaka, jambo ambalo litasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana," alisema Kifizi na kuongeza:

"Mbali na mradi huu kutoa ajira kwa vijana, pia utasaidia kuuweka mji wetu kuwa katika mazingira ya usafi, ikiwa majitaka ambayo yatakuwa yakitolewa kwenye vyoo vya wananchi yatakuwa yakipelekwe mahali ambapo ni salama tofauti na sasa ambapo humwagwa kwenye maeneo ambayo ni hatari kiafya," alisema.

Naye Ofisa Afya wa Mkoa wa Shinyanga, Neema Simba, alisema mradi huo utasaidia mkoa kutokumbwa tena na magonjwa ya mlipuko kila mara.

# Ridhiwani afunguka kero ya maji jimboni

**Na Frank Monyo**

MBUNGE wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, amesema ana imani kubwa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) kuwa itakamilisha kwa wakati mradi wa maji na kufuta historia ya kukosa huduma hiyo kwa miaka 16 katika jimbo lake.

Kauli hiyo ilitoa mwishoni mwa wiki alipotembelea kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Tanzania Steel Pipes (TSP) kilichopo Ubungo jijini Dar es Salaam kukagua mabomba yatakayotumika katika mradi wa maji wa Chalinze- Mlandizi-Mboga.

"Watu wa Chalinze kwa miaka 15 kama sio 16 wamekuwa wakisubiri huduma ya maji tangu ilivyoanzishwa awamu ya kwanza ya Wami mpaka leo hii, mambo mengi yamefanyika hapa katikati, lakini suala la upatikanaji wa maji limekuwa ni jambo la danadana, lakini tulipokubaliana na wenzetu wa Dawasa tukaamua kuanzisha mradi huu mpya jambo la faraja ni kwamba Dawasa walisema wanazopesa za kuusimamia mradi huu," alisema Kikwete.

Alisema jambo la faraja ni kwamba wakazi wa Chalinze wanaenda kuondokana na kunywa maji na mifugo na kwa mujibu wa wataalau kutoka Dawasa mradi huo hautozidi miezi mitano au sita na kwa maana hiyo watu wa Chalinze wataanza kunywa majisafi.

"Sikuwahi kuona namna wananchi wanatumia maji pamoja na wanyama kama ng'ombe ila kukamilika kwa mradi huu kutawezesha watu wangu kupata majisafi na salama ila na wao kwa upande wao nitawaomba walipie huduma ili kuweza kuendesha miradi hii maji yaweze kupatikana," alisema Ridhiwani.

Aliongeza kuwa amefurahishwa na maendeleo ya utengenezaji wa mabomba hayo, ambapo kwa taarifa aliyoipata mabomba 381 yapo tayari kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo unaotarajiwa kuanza katikati ya mwezi huu.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji Dawasa, Mhandisi Aron Joseph, alisema mradi huo hadi kukamilika utagharimu shilingi bilioni 14 na kwamba unatarajiwa kusafirisha maji lita milioni 9.3 (mita za ujazo 9300) kwa siku kiasi kinachokisiwa kuweza kutosheleza mahitaji ya walengwa kwa sasa na ongezeko la matumizi kwa siku za usoni.

"Hadi sasa, kiasi cha mabomba ya umbali wa km 3.7 yameshazalishwa katika kiwanda cha Tanzania Steel Pipes (TSP) na yameanza kupelekwa kwenye maeneo ya mradi, ambapo ujenzi unatarajiwa kuanza katika vijiji vya Mboga na Msoga," alisema Joseph.

Aliongeza katika usanifu wa mradi huo, wametilia maanani ongezeko la watu na mahitaji ya miaka 20 ijayo na kutosheleza idadi ya watu hadi kufikia 120,912 ndani ya eneo la mradi na utakuwa kwa umbali wa kilomita 58 ujenzi wa vituo viwili vya kusukumia maji na utagharimu bilioni 14 hadi kukamilika kwake.

# Mmoja afariki mgogoro wa ardhi Monduli Juu

**Na Asraji Mvungi,** MONDULI

MTU mmoja amefariki dunia na wazee sita wakazi wa Kata ya Monduli Juu, wilayani Monduli, wamenusurika kifo baada ya kushambuliwa kwa silaha za jadi wakati wakijaribu kutuliza vurugu za kugombea ardhi zilizotokea katika kata hiyo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, James Manyama, alisema jana kuwa watu wanne akiwamo Diwani wa Kata ya Monduli Juu, Baraka Sumuni, wamekamatwa kwa tuhuma za kuwa chanzo cha vurugu na wengine wanaendelea kutafutwa.

Katika tukio hilo wazee wanne kati yao walijeruhiwa vibaya kwa kukatwa sime, kupigwa mishale na marungu kichwani, mikononi na miguuni, na wawili hali zao zinaelezwa kuwa ni mbaya.

Aliyefariki ametajwa kuwa ni Simell Oltialulu mkazi wa Lendikinya.

Majeruhi wamelazwa katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru na wawili wamelazwa Hospitali ya Wilaya ya Monduli, huku wengine wawili wakiruhusiwa baada ya kupata matibabu.

Wakizungumzia tukio hilo, Tingidosoto Sima (60) na Lekisoy Mbasia, wakazi wa Kijiji cha Lendikinya ambao wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Monduli, walisema walifika eneo hilo kwa lengo la kusuluhisha mgogoro wa muda mrefu wa kugombea eneo na ghafla wakavamiwa na kundi la vijana na kuanza kuwashambulia.

"Kwa kweli hali ni mbaya na jitihada za ziada zinahitajika kwa kuwa hatua iliyofikia inatisha maana kwa kawaida kwenye jamii yetu wazee wanaheshimika sana hata kama kuna ugomvi wakisimama na kusema acha, watu wanaacha, lakini kwa hili hawakusikia wala kuheshimu," alisema Lekisoy.

Viongozi wa ngazi mbalimbali wilayani Monduli, akiwamo Mwenyekiti wa Halmashauri, Issack Joseph Kadogoo, alisema kufuatia vurugu hizo, Baraza la Madiwani limepitisha azimio la kusimamisha shughuli zote zikiwamo za kilimo katika eneo hilo hadi muafaka utakapopatikana.

Hata hivyo, Kadogoo alisema hajaridhishwa na hatua ya kukamatwa kwa Diwani wa Kata ya Monduli Juu kwa madai ya kuchochea mgogoro kwa kuwa anachokijua yeye alikuwa mmoja wa watu waliokuwa wanatafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro huo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Monduli, Julius Kalanga, alisema hatua zaidi juu ya waliohusika katika vurugu hizo zinahitajika kuchukuliwa kwa kuwa zilizochuliwa hazilingani na ukubwa wa tatizo na athari zake.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddi Kimanta, alisema watu wote waliohusika katika vurugu hizo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na wanaotumia njia ya kutengeneza migogoro kwa lengo kujinufaisha.

"Kamati ya Ulinzi na Usalama tunaendelea kukabiliana na changamoto hii ya migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara, katika baadhi ya maeneo tumefanikiwa kumaliza japo baadhi ya kata, bado tunaendelea ikiwamo kata hii ya Monduli Juu," alisema.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Jackson Leskar Sipitieck, akizungumzia utekelezaji wa Ilani ya CCM katika eneo hilo, kwenye Kata ya Loiborsiret juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tawiri wataka sensa ya tembo ifanyike

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

WATAFITI wamependekeza sensa ya tembo ifanyike mara kwa mara katika maeneo ambayo yameripotiwa kuwapo kwa kasi ya kupungua kwa idadi ya tembo

Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini (Tawiri), Dk. Edward Kohi, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki katika mahojiano maalumu na Nipashe jijini hapa.

Dk. Kohi alitaja eneo ambalo lilionekana kuwa na kasi kubwa ya kupungua kwa tembo kwa sensa ya kuwapiga picha za anga wanyamapori iliyofanyika nchi nzima kuanzia Mei hadi Novemba 2014 ni ikolojia ya Ruaha-Rungwa.

Alisema maeneo saba ya ikolojia yaliyofanyiwa sensa hiyo mbali ya Ruaha-Rungwa ni pamoja na Serengeti, Tarangire-Manyara, Katavi-Rukwa, Malagarasi-Muyovozi, Selous-Mkumi na Burigi - Biharamulo. Alisema ikolojia ya Malagarasi-Muyovozi ilionyesha tembo walipungua kwa asilimia 81 ikifuatiwa na Ruaha-Rungwa kwa asilimia 76 na Selous-Mikumi kwa asilimia 66. Alisema sensa hiyo pia ilifanyika katika maeneo ya West Kilimanjaro-Lake Natron, Hifadhi ya Taifa ya Arusha, Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na Pori Tengefu la Swaga pamoja na Ibanda-Rumanga na Kisiwa cha Rubondo.

Dk. Kohi alisema sensa hiyo ilifanyika kwa kutumia mfumo ambao ni upigaji wa picha za anga katika kundi kubwa la wanyama (TC) pamoja na mfumo wa upigaji picha za anga katika mtawanyiko wa wanyama katika eneo kubwa (SRF). Alieleza matokeo ya jumla ya sensa ya mwaka 2014 ilionyesha idadi ya tembo kwa ujumla wake walikuwa 43,521 na hivyo kupungua kwa asilimia 60 kutoka tembo 109,051 wa mwaka 2009.

Hata hivyo, Dk. Kohi alisema maeneo mawili ya ikolojia yalionyesha kuongezeka kwa tembo ambayo ni Serengeti kwa asilimia 98 na Tarangire-Manyara kwa asilimia 64.

Dk. Kohi alisema hivi sasa wapo katika hatua ya mwisho ya kutoa matokeo ya sensa ya tembo iliyofanyika nchi nzima kwa mwaka 2018.

Alisema katika kurahisisha ufanyaji wa sensa wataanza teknolojia ya ung'amuzi viumbe hai katika picha kwa kompyuta ambayo itawezesha matokeo kupatikana katika muda mfupi. Alisema teknolojia hiyo inatumia programu maalumu inayojiendesha ya kung'amua na kuwahesabu wanyamapori kupitia picha zilizopigwa kutoka angani.

Dk. Kohi alisema majaribio ya matumizi ya teknolojia hiyo ambayo yanafanyika kwa kushirikiano na Chuo Kikuu cha Glasgow cha nchini Uingereza yatafanyika mwezi ujao katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire iliyopo wilayani Babati, Mkoa wa Manyara.

## TFA yaomba ufuatiliaji waporaji mali za chama

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANACHAMA wa Chama cha Wakulima wa Tanganyika (TFA), wamemwomba Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kufuatilia uporaji wa nyumba na maghala mali ya chama kitendo alichodai kilifanywa na baadhi ya viongozi wa chama waliopita.

Katika risala ya TFA kwa Waziri Hasunga, iliyosomwa na mwenyekiti wa chama hicho, Peter Sirikwa, ilidai viongozi waliopita baada ya kupora mali zao zilizokuwa mikoa mbalimbali waliziuza kinyume cha sheria kwa maslahi binafsi.

Alidai baadhi ya viongozi hao walipora mali hizo mwaka 2016.

Aidha, tangu wakati huo, wanachama wamekuwa wakifuatilia bila mafanikio, lakini wamefarijika kuona suala hilo limeshafika Ikulu.

Alisema wanamatumaini makubwa na Rais John Magufuli kuwa atalifanyia kazi na kisha mali zao kurejeshwa.

Akifungua mkutano huo, Waziri Hasunga, aliahidi kufuatilia suala hilo.

Aidha, alikitaka chama hicho kuwekeza katika viwanda vya pembejeo na viuatilifu kwa kuwa maisha ni kilimo na viwanda.

Alisema asilimia 30.1 ya pato la taifa inategemea kilimo na huku asilimia 65.5 ya watu wakiwa wameajiriwa katika sekta hiyo kama vile wauzaji wa pembejeo, viuatilifu, na hivyo kufanya asilimia 75 ya watu kuwa katika sekta ya kilimo.

Kwa kuzingia umuhimu huo, Waziri Hasunga, alisema, wataalamu wa mbolea duniani, wanatarajia kuwasili nchini wiki hii, kufanya utafiti wa kuanzisha kiwanda cha mbolea huko Kilwa.

Alisema wataalamu hao watatembelea pia kiwanda cha mbolea cha Mijingu kilichopo wilayani Babati ili pamoja na mambo mengine kuangalia namna ya kukiboresha na kukiongezea mtaji.

Aidha, alisema wataalamu hao watafanya utafiti na kupima ardhi ili kubaini aina ya mbolea inayofaa katika eneo husika.

Alisema katika kutekeleza azima hiyo wataalamu hao watatumia gari lenye mtambo maalum wa kupima udongo ili kujua aina ya mbolea inayotakiwa kila eneo badala ya matumizi ya mbolea moja kwa madai kuwa inafaa kwa eneo kubwa la ardhi.

Alisema azima ya serikali ni kutaka mbolea yote izalishwe hapa hapa nchini.





# Mjane aliyepokwa mali arudishiwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MJANE Agness Abraham (34), mkazi wa Kijiji cha Mlima Shabaha katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro ambaye alipokwa mali mbalimbali yakiwamo mashamba, mifugo na nyumba na watu ambao ni ndugu wa mumewe, amefanikiwa kurejesha mali hizo baada ya wasaidizi wa kisheria kuwabana kwa Sheria ya Mirathi.

Agness ambaye alikuwa mke mdogo wanne wa Abraham Mollel, aliporwa kwa nguvu mali hizo mwaka jana na watoto wakubwa wa marehemu pamoja na viongozi wa koo wa jamii ya wafugaji wa Kimasai, huku akiachiwa kulea watoto wanne ambao wana umri chini ya miaka 18.

Akieleza kufurahishwa kwake na ushindi huo, mjane Agness alisema alipokwa mali hizo muda mfupi baada ya mumewe kufariki dunia mwaka 2013 na watoto wakubwa wa mke wa kwanza walioteuliwa na wazee wa ukoo kusimamia mirathi, walimwondoa katika orodha ya mgawanyo wa mali alizochuma na mumewe wakati akiwa ahai.

"Hawakunipa chochote, walichukua kila kitu alichoacha marehemu mume wangu katika nyumba niliyokuwa naishi, walikataa watoto na nikaishi nao kwa tabu wakati natafuta haki yangu na wanangu. Hawakutaka watoto wangu wapate huduma za afya na elimu kwa jina la baba yao, wakaninyang'anya hadi shamba langu ili nisizalishe chakula," ameeleza mjane huyo.

Alisema ilimchukua muda kuamini, lakini alipoamua kwenda kwa mzee wa ukoo kuhoji zaidi hatima yake, akaelezwa kwamba wanaostahili kurithi mali wameshachukua chao na kama yeye hajapata, basi si sehemu ya familia ya marehemu.

Baada ya kuona haki yake inataka kupotea, alikutana na Wasaidizi wa Kisheria, Elimu Makere na Eutropia Assenga, ambao walimtia moyo na kumpatia elimu ya msaada wa ushauri wa kisheria kuhusu sheria za mirathi, ndoa na wosia na hatua wanazoweza kuchukua kuhakikisha mjane huyo anapata haki yake kwa mujibu wa sheria.

Akielezea zaidi kuhusu kisa hicho, mmoja wa Wasaidizi wa Kisheria katika Wilaya ya Hai, Assenga alisema baada ya kupata taarifa za mjane huyo kunyanyaswa na kupokwa mali, walimfuata na kumpa elimu kuhusu mgawanyo wa mali na utaratibu wa mila na desturi za wafugaji wa jamii ya Kimasai na baadaye wakawaita wahusika katika familia hiyo na kuwabana ili kurejesha mali za mjane huyo.

"Tulilazimika kuita viongozi wa ukoo, watoto wakubwa wa mzee Abraham na kuwaeleza namna mwanamke anavyoweza kumiliki mali za ndoa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na Sheria ya Ardhi, Namba 5 ya Mwaka 1999. Tulivyowaeleza hizo taratibu za kisheria walikataa na baadaye tulipowaambia tunakwenda mahakamani na tutamsaidia kila kitu huyo mjane, wazee wakasema ngoja waende wakazungumze nje, na waliporejea wakasema wamekubali kumrudishia mali zake," alisema.

Kwa mujibu wa msaidizi huyo wa kisheria, mali zilizorejeshwa ni ng'ombe wanane, shamba analolima mahindi na maharage lenye ukubwa wa ekari nne na nyumba aliyokuwa amejengewa na mumewe kabla ya umauti kumkuta.

Kazi ya kuwaongoza na kuwanoa wasaidizi hao wa kisheria katika Mkoa wa Kilimanjaro, inatekelezwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility (LSF).

Akifafanua zaidi kuhusu mkasa huo, Makere ambaye naye ni msaidizi wa kisheria alisema: "Tulifanikiwa kuwashika pabaya, hasa pale tulipowaeleza madhara ya sheria hizo kama wataendelea kushikilia mali za mjane huyo. Tukawaambia pia watoto wale wameshindwa kwenda shule kwa sababu wananyanyasika, tutachukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Mtoto ya mwaka 2009, wakaishiwa nguvu na kukubali kuandikisha kwa maandishi kurejesha mali hizo na sasa mama huyo ameshakabidhiwa mali zake."



Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema) Tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi, akisoma utaratibu wa wamiliki wa migodi kuorodhesha majina ya wafanyakazi wao migodini juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali kuweka minara ya mawasiliano mipakani

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

SERIKALI imesema itaweka minara ya redio na mawasiliano ya simu za mkononi katika maeneo ya mpakani yanayozitenganisha nchi za Tanzania na Kenya ili kumaliza tatizo la wakazi wa Tarakea na Holili katika Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro kukosa mawasiliano ya mtandao huo kwenye nchi waliyozaliwa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Ujenzi na Mawasiliano, Dk. Jimmy Yonazi, ameyasema hayo jana, wakati alipofanya ziara ya kutembelea vijiji vilivyopo mpakani na nchi jirani ya Kenya katika upande wa Wilaya ya Rombo.

"Licha ya kuwapo kwa changamoto hii ya wananchi wetu kusikiliza redio za Kenya na kupata mawasiliano ya mtandao wa simu kutoka nchi jirani, niwahakikishie tu wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kwamba serikali ina nia ya kuweka minara ya mawasiliano wakati wowote kuanzia sasa ili kumaliza adha mnayoipata," alisema.

Dk. Yonazi amewatoa hofu wananchi wanaopata adha ya mawasiliano hayo, akisema serikali itaweka minara ya redio na simu katika maeneo ambayo hayana mawasiliano, licha ya changamoto kubwa maeneo kadhaa kuwapo nyuma ya Mlima Kilimanjaro ambao unazuia masafa kuwafikia wananchi vizuri.

Baada ya kufika katika lango la mpaka wa Tarakea, viongozi hao walishuhudia wingi wa maduka ya muda ya nchi jirani yanayotoa huduma za mawasiliano na huduma za fedha.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, Peter Ulanga, akizungumza na wananchi wa maeneo hayo mbele ya Naibu Katibu Mkuu huyo, aliwatoa hofu wananchi hao akieleza kuwa jambo hilo litamalizwa na serikali ya awamu ya tano ambayo imedhamiria kuwaunganisha pamoja wananchi wake.

Alisema mawasiliano hayo ya mitandao ya simu na redio, hayafiki katika vijiji vilivyopo mipaka ya Holili na Tarakea na baadhi ya vijiji vilivyopo nyuma ya mlima huo kutokana na Mlima Kilimanjaro kuzidi urefu wa masafa.

Hata hivyo, wananchi wa Tarakea waliwaeleza viongozi hao kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wanalazimika kutumia mitandao ya nchi jirani ya Kenya kufanya mawasiliano na huduma za fedha.

"Tunafanya hivyo kwa sababu redio za nchi ya Kenya ndio zinazosikika vizuri mpakani na redio za Tanzania hazipatikani masafa yake. Sasa kwa sababu mmekuja wenyewe, tuiombe serikali itufetee huduma za mawasiliano ya simu na redio ili kupata taarifa mbalimbali na vipindi vya Tanzania," alisisitiza John Shirima.

Awali, Katibu Tawala wa Wilaya ya Rombo, Abubakar Asenga, alisema katika wilaya hiyo hakuna redio inayopatikana katika vijiji vya maeneo ya mpakani pamoja na pembezoni.

# Wamaliza minong'ono ya kuuzwa shule

**Na Paul William,** MWANGA

MWENYEKITI wa Taifa wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Dk. Edmund Mndolwa, amemaliza minong'ono kuhusu madai ya shule kutaka kuuzwa kwa baadhi ya shule zake za sekondari nchini kwa kile kinachoelezwa ni kushindwa kujiendesha, akisema hawana mpango huo.

Dk. Mndolwa alimaliza minong'ono hiyo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, wakati wa mahafali ya 10 ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari ya Mwanga.

"Niwaeleze wale wanaosubiri tuuze, kwamba kwa sasa hatuna mpango wa kuuza shule zetu za sekondari ambazo tunamiliki na badala yake tutaziboresha ili kutoa elimu yenye ushindani. Lakini pia tutazibadili matumizi baadhi ya shule na kuwa vyuo vya ufundi, huo ndio msimamo wetu kama jumuiya," alisema.

Pia, jumuiya hiyo imewataka wale wote ambao walinunua shule za jumuiya hiyo na wako tayari kuzirejesha kwao, kufanya hivyo mara moja.

Dk. Mndolwa alikiri kuwa katika kipindi cha nyuma kulikuwapo na mpango wa kuuza shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo na baadhi kuuzwa.

Alisema katika uongozi wake, hakuna shule itakayouzwa, lakini ili kuendana na malengo ya Serikali ya Tanzania ya Viwanda, wanao wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanazalisha wataalamu wa kutosha kupitia shule za ufundi za Jumuiya ya Wazazi.

"Changamoto iliyokuwa ikizikabili shule zinazomilikiwa na jumuiya hii ni tabia ya baadhi ya viongozi na walimu kujinufaisha kupitia makusanyo ya fedha na mali za shule. Mimi niahidi hapa kwamba tumeshajipanga kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa katika shule hizi zinarudi na kunufaisha shule na sio watu binafsi," alisisitiza Dk. Mndolwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Jumuiya Taifa, Erasto Sima, alisema shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo ambazo hazina maendeleo mazuri, wamegundua chanzo chake ni ubovu wa bodi za shule pamoja na ubovu wa walimu wakuu.

"Kibaya zaidi wamekuwa hawapeleki makato mbalimbali NSSF (Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii) na TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), hivyo kusababisha shule kuwa na madeni makubwa ikilinganishwa na uwezo wa shule. Na siku wakiondoka madeni hayo yanabaki kuwa ya jumuiya ya wazazi ambao ndio wamiliki," Sima alisema.

NIPASHE JUMATATU APRILI 1, 2019
Nipashe

# Spotika



WACHEZAJI WENYE THAMANI KUBWA EPL MSIMU 2018-19 UK.16



## ISIKUPITE

Lionel Messi ameifikia rekodi ya kipa wa zamani wa Real Madrid, Iker Casillas ya kuwa sehemu ya ushindi kwenye mechi 334 za La Liga, akikamilisha rekodi hiyo wakati Barcelona ikiwachapa mahasimu wao wa Catalunya, Espanyol juzi, Jumapili. Rekodi hiyo inakuja wakati akitoka kuipiku ile ya Andres Iniesta, kwa kuwa mchezaji wa pili Barca aliyecheza mechi nyingi zaidi baada ya kushuka dimbani mara 675 akiwa na 'Blaugrana' hao, akiwa safari ndefu kuweza kumfikia kinara Xavi aliyeichezea mechi 767.



## JUU KWA JUU...

Mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus (kushoto), katika harakati za kuwania mpira wa juu na beki wa kushoto wa Fulham, Maxime Le Marchand, kwenye mechi ya Ligi Kuu England juzi, Jumapili wakati City ikishinda 2-0. **PICHA: REUTERS**

SOKA



# WA4 WENYE MIKONO YA MOURINHO, GUARDIOLA

**LONDON,** England

HUWEZI kuacha kusema kwamba, Jose Mourinho na Pep Guardiola ni makocha wawili bora zaidi Ulaya kwa wakati huu. Mashabiki wa Ligi Kuu ya Egland, EPL, wana bahati kuwaona wote wawili wakiwa pamoja England.

**Makocha wote hawa wawili walipata ujuzi wao kwa miamba wa soka la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, pale Catalan kwa Barcelona, wakianza kama makocha wasaidizi. Wamekuwa makocha wenye mafanikio makubwa katika kazi zao na klabu kadhaa kuhitaji huduma yao, huku pia wachezaji wengi nyota wamekuwa na ndoto ya kucheza chini yao.**

Makocha hao wote wawili, Mourinho na Guardiola wamewanoa wachezaji bora zaidi duniani, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wakicheza chini yao. Lakini, wamekuwa wachezaji wachache wenye bahati ya kupata bahati ya kucheza chini ya makocha wote wawili katika klabu tofauti.

Hapa tunawaangalia wachezaji ambao walicheza chini ya Mourinho na Guardiola katika klabu tofauti.

**1. ALEXIS SANCHEZ**

Alexis Sanchez, kwa sasa akiwa anavaa jezi namba saba anacheza soka lake pale Old Trafford. Aliichezea kwanza Barcelona kabla ya kuhamia klabu ya Ligi Kuu ya England, Arsenal na kisha Manchester United. Sanchez alisajiliwa na Pep Guardiola pale Barcelona mwaka 2011, baada ya kuwa na msimu mzuri kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Alikuwa mchezaji wa kwanza kutoka nchini Chile kucheza pale Camp Nou na aliingizwa kwenye kikosi cha timu ya kwanza na Guardiola.

"Sanchez ni kijana sana," alisema akiiambia BBC.

"Anaweza kucheza katika nafasi zote tatu za ushambuliaji, anaonesha ujuzi wa kulinda na kumiliki mpira, ni kijana mzuri zaidi."

Sanchez alikaa hapo Nou Camp na Guardiola kwa msimu mmoja na alifunga mabao 12. Baada ya Guardiola kuondoka Barcelona, Sanchez alikaa misimu miwili nchini Hispania na mwishoni akajiunga na Arsenal mwaka 2014. Uwezo wake wa kufunga mabao pale Arsenal ulimvutia Jose Mourinho, ambaye alimsajili kutoka kwa mpinzani wake mkubwa Arsene Wenger wakati wa dirisha dogo la Januari. Kitu tunachoweza kusema ni kwamba alikuwa anacheza vizuri zaidi chini ya Mhispania na bado hakuweza kuwa kwenye kiwango chake chini ya kocha Mourinho na sasa Ole Gunnar Solskjaer.

**2. CESC FABREGAS**

Cesc Fabregas, ni zao la kituo cha kulelea vipaji cha La Masia pale Barcelona, lakini alianza kucheza soka lake la kulipwa akiwa na Arsenal kwenye Ligi Kuu England. Baada ya misimu nane na 'Washika Bunduki' hao, alikwenda kucheza Barcelona na sasa Chelsea.

Alirudishwa pale Camp Nou na Pep Guardiola mwaka 2011 kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 29. Alijitengenezea nafasi yake pale Barcelona kwenye nafasi ya kiungo ambapo tayari kulikuwa na wakali kama Iniesta, Xavi na Busquets ambao wote walikuwa kwenye kiwango cha juu kabisa.

Baada ya kucheza kwa mafanikio kwa misimu mitatu katika klabu yake hiyo ya utotoni, alikubali kurudi England na safari hii chini ya Jose Mourinho akiwa Chelsea mwaka 2014. Alipata mafanikio kwenye msimu wake wa kwanza hapo Stamford Bridge, akishinda taji la Ligi Kuu na kuwa mmoja wa waliotoa pasi za mwisho nyingi zaidi kwa msimu mzima.

Mhispania huyo alikuwa na wakati mzuri zaidi katika nafasi ya kiungo chini ya makocha wote wawili, lakini muda wake chini ya Mourinho unaweza kutajwa kama ndio uliokuwa na mafanikio zaidi kwake.

**3. PEDRO**

Pedro alikuwa ni mchezaji ambaye alipandishwa na Pep Guardiola kwenye kikosi cha kwanza cha Barcelona mwaka 2009, akimtumia kama mchezaji wa akiba. Winga huyo ambaye kwa sasa anacheza pale Chelsea, alikuwa chaguo la kwanza chini ya Guardiola kwa muda wake wote Camp Nou, akishinda taji la La Liga na akishinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu wa 2009-10.

Alikuwa nguzo muhimu zaidi wakati Barca ikishinda mataji matatu mwaka 2015, lakini nafasi yake ya kuanza kucheza mara kwa mara ikapungua baada ya kutua kwa Alexis Sanchez mwaka 2011.

Hivyo, baada ya kuwa na mafanikio na klabu yake hiyo ya utotoni, ambako alishinda kila taji, alisajiliwa na Mourinho katika klabu ya Chelsea kipindi cha majira ya joto 2015. Haraka Blues hao wakamfanya kuwa ndio mchezaji wao namba 11 wa kudumu hapo Stamford Bridge, akifunga bao katika mchezo wake wa kwanza na klabu hiyo.

Alikaa miezi sita tu na 'Special One' huyo, lakini kwa kipindi kifupi kilimwonyesha kuwa nguzo muhimu zaidi kati ya makocha wote wawili Guardiola na Mourinho.

Katika mahojiano yake na Gazeti la Mirror mwaka 2015 alipoulizwa kuhusu makocha hao wawili alisema: "Kwa kazi, wote Mourinho na Guardiola wanafanana. Hawataki morali kushuka hata kwa dakika moja."

**4. KEVIN DE BRUYNE**

Pengine mchezaji bora zaidi kuwahi kufundishwa na makocha wote wawili, Mourinho na Guardiola ni Kevin De Bruyne. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji tayari alikuwa mchezaji wa Chelsea kabla ya Mourinho hajachukua nafasi ya kuinoa timu hiyo ya Stamford Bridge mwaka 2013.


Chini ya Mreno huyo, De Bruyne alianza katika mechi tatu tu za Ligi Kuu kwa Blues na mwishoni mwa mwaka 2013, ilikuwa wazi kwamba Mbelgiji huyo alikuwa anaondoka kwa kuwa hakuwa kwenye mipango ijayo ya Mourinho hapo Chelsea.

Mourinho, ambaye alikuwa kocha wa Manchester United, alisema kwa wakati huo: "Najaribu kuwa mkweli kwa Kevin. Hajachaguliwa kwa sababu sikupenda jinsi alivyocheza kwenye mchezo dhidi ya Swindon na sikuridhishwa na jinsi alivyokuwa akifanya kwenye mazoezi."

Hivyo, aliondoka klabuni hapo mwaka 2014, na alipotua Manchester City akawa kiungo wa kiwango cha juu na akajiunga na mpizani wa Mourinho, Guardiola pale kwenye dimba la Etihad.

De Bruyne alikuwa nyota chini ya Guardiola, wakati hakupewa nafasi chini ya Mourinho.

**JE, WAJUA?**



Sergio Aguero amehusika katika mabao nane kwenye mechi tano zilizopita za ligi dhidi ya Fulham (mabao matano, pasi za mwisho tatu).

## NJE YA UWANJA

# Zidane amweka Bale njia panda

ZINEDINE Zidane amekataa kuthibitisha endapo Gareth Bale atakuwapo katika kikosi chake cha Real Madrid msimu ujao, lakini akafunguka kuwa atakuwa sehemu ya kikosi chake muhimu wiki hizi za mwisho wa msimu.

Tetesi za mustakabali wa baadaye wa Bale hapo Santiago Bernabeu zimekuwa za kukatisha tamaa kwa msimu huu ambao Madrid imekuwa ikihaha tangu kuondoka kwa Cristiano Ronaldo na kujiunga na Juventus.

Lakini Zidane hakutaka kuweka wazi kuhusu mustakabali wa nyota huyo wa kimataifa wa Wales katika mkutano na waandishi wa habari jana, Jumapili kabla ya kuivaa Huesca, ila akaeleza kuwa ni sehemu ya kikosi chake kwenye mechi zilizobaki msimu huu wa 2018-19.

"Tunakwenda kucheza mechi hizi 10 na kisha tutaona," Zidane alisema wakati alipoulizwa kuhusu Bale.

"Sitazungumza kuhusu msimu ujao, tunazo mechi 10 zilizobaki. Gareth ni memba muhimu katika kikosi hiki, tunajua nini alichokifanya hapa, zaidi kwenye mechi ya fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Hakuna mtu anayeweza kuondoa kile alichokifanya. Tunajua anaweza kuleta mengi kwa timu na tutamhesabu. "




# CECAFA ILIVYOWEKA REKODI AFCON 2019



Wachezaji wa Taifa Stars wakishangilia baada ya mechi yao dhidi ya Uganda kumalizika kwa ushindi wa mabao 3-0, na kufuzu Afcon 2019.

**Na Adam Fungamwangwo**

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya soka, Ukanda wa Afrika Mashariki, maarufu kama Baraza la Soka Afrika Mashariki (Cecafa), umepeleka timu nne kwenye fainali za Mataifa Afrika (Afcon) zitakazofanyika Juni mwaka huu nchini Misri.

> **Ukanda wa Afrika Mashariki, unaoongozwa na Cecafa, awali ulikuwa ukichukuliwa kuwa ni ukanda duni kwenye viwango vya soka Afrika, lakini kwa sasa unaonekana kuinuka kwa kasi na kugeuka kuwa tishio.**

Ni nadra sana kwa nchi za Ukanda wa Cecafa kupeleka timu Afcon, lakini inapotokea hivyo baada ya miaka kadhaa inayofanikiwa huwa ni nchi moja tu, na baada ya hapo hali ya ukame inaendelea kama kawaida.

Wakati Watanzania wakiwa na furaha kubwa baada ya timu ya Tanzania, 'Taifa Stars' kufuzu kwa mara ya kwanza baada ya miaka 40, timu zingine tatu za Ukanda wa Cecafa zimefanikiwa kufuzu na kuziacha nyingi za kanda mbalimbali za Kusini, Kaskazini na Magharibi zikishindwa kuingia fainali hizo.

Zifuatazo ni timu zote kutoka nchi nne za Afrika Mashariki na safari zao ndefu hadi kufanikiwa kutinga Afcon kwa idadi hiyo kwa mara ya kwanza kwenye historia ya michuano hiyo mikubwa barani Afrika.

**1. BURUNDI**

Timu ya Taifa ya Burundi 'Intamba Murugamba' ni moja kati ya timu zilizoingia kwenye fainali za Mataifa ya Afrika Afcon kutoka kwenye Ukanda wa Cecafa. Imetinga kwa mara ya kwanza kwenye historia ya taifa hilo.

Imefanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kujikusanyia pointi 10 kwenye Kundi C na kushika nafasi ya pili nyuma ya Mali iliyomaliza kinara ikiwa na pointi 14. Imetinga hatua hiyo ikiipiga kumbo timu ya Taifa ya Gabon iliyokuwa ikipewa nafasi kubwa, chini ya straika hatari anayeichezea Arsenal, Pierre Emerick Aubameyang.

Ilianza nyumbani mechi zake kwa kuitwanga Sudan Kusini mabao 3-0, sare ya 1-1 ugenini nchini Gabon, na sare ya bila kufungana dhidi ya Mali ugenini pia. Baada ya hapo ikalazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Mali, ikaitwanga Sudan Kusini ugenini mabao 5-2, kabla ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Gabon na kuiwezesha kufuzu.

**2. KENYA**

Ukanda wa Cecafa umefanikiwa kupeleka timu nyingine ya pili ambayo ni Kenya. Timu ya Taifa ya Kenya, 'Harambee Stars' imefuzu Afcon kwa kukamata nafasi ya pili kwenye Kundi F na kuyapiga kumbo mataifa ya Ethiopia na Sierra Leone.

Kenya ilivuna pointi saba ikiwa nyuma ya Ghana iliyoongoza kundi kwa kuwa na pointi tisa. Kundi lilianza kwa mkosi baada ya Sierra Leone kujitoa, likabaki na timu tatu tu.

Mechi ya kwanza iliichapa Ghana nyumbani bao 1-0, kabla ya sare ya bila kufungana ugenini dhidi ya Ethiopia. Baada ya hapo ikaachia kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Ethiopia, kabla ya kufungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Ghana, lakini pointi zake zikawa zimeiwezesha tayari kutinga Afcon.

**3. UGANDA**

Ndiyo timu pekee ya Ukanda wa Cecafa ambayo imetinga Afcon kwa kuongoza kundi. Uganda 'Cranes', imekuwa kinara wa Kundi L ikiwa imejikusanyia pointi 13. Ilianza kampeni yake hiyo kwa kuitwanga Cape Verde ugenini bao 1-0, kabla ya kulazimishwa sare ya bila kufungana nyumbani na Taifa Stars.

Baada ya hapo ilicharuka na kuitwanga Lesotho mabao 3-0 nyumbani, lakini pia ikaenda kuifunga timu hiyo hiyo ya Lesotho mabao 2-0 ugenini. Uganda ikaichapa tena Cape Verde nyumbani, kabla ya kusasambuliwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Tanzania. Hata hivyo, tayari ilikuwa imeshafuzu.

**4. TANZANIA**

Tanzania ama Taifa Stars. Imefuzu Afcon baada ya miaka 40. Mara ya mwisho kufuzu ilikuwa ni 1979 ilipofuzu ikiwa ugenini nchini Zambia kwa kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KK Eleven ikiitwa wakati ikiwa ni kifupi cha jina la Rais wa Kwanza wa nchini hiyo, Kenneth Kaunda, lakini sasa inaitwa Chipolopolo. Mechi hiyo ilichezwa Novemba 11, 1979 nchini Zambia.

Zikiwa zimesalia dakika chache mpira kumalizika, straika hatari wakati huo, Peter Tino alisawazisha bao ambalo Zambia ililipata kupitia kwa Alex Chola.

Sare hiyo iliifanya Stars ifuzu kwa sababu katika mechi ya kwanza iliyochezwa Tanzania Oktoba 28, ilishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Mohamed Rishald Adolf ambaye kwa sasa ni Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons ya Mbeya, hivyo matokeo ya jumla yakawa ni mabao 2-1. Fainali zake zilichezwa nchini Nigeria mwaka 1980. Mwaka huu Stars imefanikiwa kutinga Afcon baada ya kushika nafasi ya pili kwenye Kundi L ikiwa na pointi nane, likiongozwa na Uganda iliyomaliza na pointi 13.

Ilianza kwa sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Lesotho, kabla ya kulazimisha sare ya bila kufungana ugenini dhidi ya Uganda.

Ikachapwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Cape Verde, lakini ikaichapa timu hiyo hiyo mabao 2-0 nyumbani, na kwenda kulala 1-0 ugenini dhidi ya Lesotho kabla ya kuitungua Uganda mabao 3-0 nyumbani na kutinga hatua hiyo.

**ZITAFANYA VEMA KWENYE FAINALI?**

Hata hivyo, mashabiki wengi wanajiuliza kama timu hizo za Afrika Mashariki endapo zitakwenda kufanya vizuri kwenye michuano hiyo au zinatakuwa wasindikizaji? Muda utaongea.

## Extra Time

# WACHEZAJI WENYE THAMANI KUBWA EPL MSIMU 2018-19



EDEN HAZARD

**LONDON,** England

SOKO la uhamisho wa wachezaji limepanda thamani kwa kipindi cha miaka michache. Na imekuwa kama mchezo, kwani mchezaji X akiwa na thamani kubwa basi mchezaji Y atakuwa na thamani kubwa zaidi.

**Itawezekana kweli mchezaji kuja kununuliwa kwa pauni milioni 500? Unaweza kudhani ni jambo la kushangaza. Lakini ngoja nikurudishe nyuma kidogo hadi kipindi cha majira ya joto mwaka 2002, wakati Rio Ferdinand aliposajiliwa na Manchester United kwa pauni milioni 30.**

Ilikuwa ni ada iliyovunja rekodi kwa wakati ule, hakuna mtu ambaye angeamini kwamba kiasi kile cha fedha kingetumika kumnunua mchezaji. Halafu likaja suala la Fernando Torres wakati alipohamia Chelsea kwa pauni milioni 50 mwaka 2011, tena kila mmoja alishtuka.

Ingawa sasa tunawaona wachezaji kama Phillipe Coutinho akienda Barcelona kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 105.

Sasa katika orodha hii tunakuchambulia wachezaji wenye thamani kubwa, ambapo wengine wanaweza kukushangaza na wengine utaona kwamba wanastahili.

### 10. ROMELU LUKAKU (MAN UNITED) – PAUNI MILIONI 76.5

Ni zao la akademi ya vijana ya Anderlecht, Romelu Lukaku amefanya mabadiliko makubwa kwenye soka katika siku za sasa. Nguvu zake zimemfanya kuwa mmoja wa washambuliaji hodari na wakali zaidi dimbani. Ni ngumu kwa mchezaji kuwa na nguvu na kasi kwa wakati mmoja.

Uhamisho wa kwanza mkubwa wa Lukaku ulifanyika mwaka 2011, wakati aliposajiliwa pale Chelsea kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 13.5 akiwa na umri wa miaka 18 tu wakati huo, akapelekwa kwa mkopo West Bromwich Albion, ambako alifunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu England. Kipaji chake sasa hakikubainishwa wazi na Mourinho akamwondoa kwenye kikosi cha kwanza. Na matokeo yake Lukaku alipelekwa tena kwa mkopo Everton.

Bado, Lukaku akafunga mabao 15 katika mechi 31, alizowacheza 'Toffees' hao wakatoa ofa kwake. Ada ya awali ilikuwa ni pauni milioni 25.

Kwa kipindi cha misimu mitatu aliyokaa Everton, Lukaku aliweza kufunga mabao 53 katika mechi 110. Na Manchester United ikamuona.

Alikuwa ni Jose Mourinho, mtu ambaye hakuonyesha kumhitaji wakati akiwa Chelsea, na akamsajili kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2017. Mwisho wa siku akasajiliwa kwa pauni milioni 75 na sasa thamani yake imepanda zaidi.

### 9. PAUL POGBA (MAN UNITED) – PAUNI MIL 81.

Kwa mara ya kwanza Manchester United ilimkataa, Paul Pogba wakati akiwa ndio kwanza kinda.

Baada ya kusajiliwa na United mwaka 2009 akitokea timu ya Le Havre ya kikosi cha wachezaji chini ya umri wa miaka 19, Pogba hakupata nafasi ya kucheza kwa muda mrefu.

Kocha, Sir Alex Ferguson aliamua kuachana naye na alijiunga na Juventus kwa uhamisho huru.

Maisha ya Pogba kule Juventus yalikuwa ya kuvutia. Akashinda mataji mawili ya Italia, mawili ya Italian Super na manne ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A. Na hapo mambo yakamnyookea Pogba na kuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa wakitazamwa zaidi Ulaya. Kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2016 United ikamsajili tena.

Ada yake ilikuwa ni kubwa zaidi tofauti na mwanzo, kwani sasa thamani yake ikaongezeka mara dufu.

### 8. DELE ALLI (TOTTENHAM HOTSPUR) – PAUNI MIL 90

Dele Alli wakati anahama kutoka timu ya MK Dons kwenye Spurs Januari mwaka 2015 ada yake ilikuwa ni pauni milioni sita. Halafu baadaye akarudishwa tena Dons kucheza kwa mkopo, kabla ya kurudi moja kwa moja Tottenham.

Alli akajiimarisha mwenyewe na kuwa katika kikosi cha kwanza cha Spurs na akacheza mechi 33 katika michezo 38 akifunga jumla ya mabao 10.

Tangu hapo Alli amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa Spurs na timu ya Taifa ya England. Kwa sababu amekuwa na namba ya kudumu na sasa soko lake limekuwa kubwa na thamani yake imefikia pauni milioni 90. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amekuwa bidhaa muhimu kwa klabu yake na klabu kadhaa zimekuwa zikimtolea macho.

### 7. N'GOLO KANTE (CHELSEA) – PAUNI MIL 90

Kila mmoja kwa sasa anamjua vizuri N'Golo Kante hasa kutoka na kile anachokifanya akiwa dimbani.

Baada ya kusajiliwa Leicester kipindi cha majira ya joto mwaka 2015 kwa pauni milioni nane. Kante amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho. Hakuna mtu ambaye alimtarajia.

Alibeba taji la Ligi Kuu kwa mara ya kwanza akiwa na Leicester na Chelsea ikamsajili kwa pauni milioni 30.

Tangu hapo amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwenye kikosi cha Chelsea na thamani yake imepanda hadi kuwa pauni milioni 90.

### 6. LEROY SANE (MAN CITY) – PAUNI MIL. 90

Leroy Sane alikuwa mmoja wa vijana wadogo wenye vipaji vya ukweli kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wakati Manchester City iliposamjili kwa pauni milioni 45 kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 akitokea Schalke. Kila mmoja alijua kwamba ataweza kuwa na wakati mzuri zaidi hapo Man City.

Na ndivyo ambavyo amejithibitisha yeye mwenyewe, kwani kwa sasa amekuwa mmoja wachezaji muhimu wa Manchester City na thamani yake imepanda hadi kuwa pauni milioni 90.

### 5. RAHEEM STERLING (MAN CITY) – PAUNI MIL 108

Kwa sasa ni mmoja wachezaji muhimu zaidi kwa Manchester City, kwani thamani imepanda maradufu hadi kufikia pauni milioni 108.

Awali alianza kucheza katika Klabu ya Queen's Park Rangers katika timu ya vijana na baadaye akasajiliwa Liverpool.

Alikaa na Liverpool kwa misimu mitatu na alionyesha kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa kikosi hicho.

Baada ya kuonyesha kiwango cha juu, Sterling alisajiliwa na Manchester City kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 60 kipindi cha majira ya joto.

### 3. EDEN HAZARD (CHELSEA) – PAUNI MIL 135

Kwa muda sasa, Eden Hazard amekuwa mchezaji muhimu kwa klabu yake na timu ya Taifa ya Ubelgiji.

Alitua Chelsea mwaka 2012, akitokea Ufaransa na thamani yake ikipanda siku hadi siku. Kwa sasa Real Madrid ndio inatajwa zaidi kuwani saini yake, huku thamani yake ikizidi kupaa.

### 2. HARRY KANE (TOTTENHAM HOTSPUR) – PAUNI MIL 135

Kwa sasa anatajwa kuwa mshambuliaji bora wa England. Wakati akiwa na umri wa miaka 18, alipelekwa kucheza kwa mkopo pale Leyton Orient. Kane baadaye akapelekwa tena kucheza kwa mkopo kule Millwall.

Halafu tena akapelekwa Norwich City na baadaye Leicester City, kabla ya kurudi tena Spurs akiwa na umri wa miaka 20.

Kane kwa kipindi cha misimu sita iliyopita amecheza mechi 125 na kufunga mabao 175, huku thamani yake ikipanda hadi kufikia pauni milioni 135. Kwa sasa ni nahodha wa timu ya Taifa ya England na alikuwa mfungaji bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana.

### 1. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL) – PAUNI MIL 135

Mohamed Salah kwa sasa yupo kwenye kilele cha mafanikio yake katika soka. Amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa timu ya Liverpool na thamani yake imepanda kwa kasi. Awali alicheza pale Chelsea kabla ya kwenda AS Roma ya Italia, akiwa pia amecheza kwa mkopo Fiorentina.

Kipaji chake kwa sasa ni cha aina yake akiwa na thamani kubwa zaidi, kwani anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 135.

## Nukuu

"Kocha aliyenifuatia baada yangu mimi ambaye alikuwa [Jose] Mourinho alibadilisha staili, kwa sasa kuna kocha ambaye anapaki basi na kucheza mashambulizi ya kushtukiza, lakini tofauti kubwa iliyopo kati ya Mourinho na [Ole Gunnar] Solskjaer ni kwamba Solskjaer anashinda, mimi siko pale, lakini hali inaonekana imetulia kwa sasa na mazingira yamekuwa mazuri," **Kocha wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal, aliiambia BBC.**



"Mabadiliko yanaweza kuleta hali chanya, tulikuwa na wakati wa kufurahisha chini ya Zizou [Zinedine Zidane] na ni furaha tena kurudi nyumbani, kurudi kwake imekuwa habari njema kwa wachezaji wote, hayakuwa maamuzi yangu kumleta tena hapa, hata kama watu wanafikiri hivyo. Mimi ni nahodha na huwa natoa mawazo yangu kama nikiombwa; siwezi kulazimisha, au kufanya ninachotaka," **Sergio Ramos akizungumza na wanahabari kufuatia madai kuwa yeye ndiye kashawishi Zidane arejeshwe Real Madrid**



"Kwa kweli jana nilifurahi sana jinsi mlivyokuwa mnacheza na jinsi mlivyofunga magoli, Watanzania wanataka furaha, sio kufungwafungwa kama mlivyofungwa kule Lesotho, ile iliniuma sana hadi nilipanga kuwa sitaita tena timu kuja hapa Ikulu, lakini sasa safi. Nataka niwahakikishie serikali ipo nanyi na ni matarajio yangu kuwa mtajiandaa vizuri ili mkafanye vizuri katika michuano ya Afcon huko Misri, sasa vita imeanza," **Rais John Magufuli akizungumza na wachezaji wa Taifa Stars baada ya kuifunga Uganda 3-0 na kufuzu Afcon 2019.**



Michezo




# GINIKI AVYOZIMA WAKENYA tiGO KILI HALF MARATHON

Mshindi wa mbio za kilomita 21 maarufu kama tiGO Kili Half Marathon, Emmanuel Giniki, akimaliza mbio hizo huku akishangiliwa na umati wa mashabiki katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi mwezi uliopita.

**Na Mwandishi Wetu**

"UZOEFU na roho ngumu katika kuhakikisha nafanya kazi na matokeo ninayaona, ndicho kilichoniwezesha kuibuka mshindi wa kwanza Tigo Kili Half Marathon," ndivyo anavyoanza kusimulia mwanariandha Mtanzania Emmanuel Giniki, anayetingisha kwa sasa katika riadha alipoketi na Nipashe kutaka kujua siri ya mafanikio yake.

**Giniki alitumia saa 1:03:34 kwenye mashindano hayo yaliyofanyika mjini Moshi na kufanikiwa kuwabwaga wanariadha wa Kenya wanaoonekana kutawala katika kinyang'anyiro hicho, takriban kila mwaka.**

Katika mahojiano maalum na Mwandishi Wetu, Giniki mwanariadha wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), anasema tangu walipoanza kukimbia mapema asubuhi siku hiyo, hakuwahofia wanariadha kutoka Kenya.

"Unajua mwanzo mnapoanza kukimbia kila mtu hujitahidi kwa kuwa bado anakuwa na nguvu. Lakini kadri unavyokwenda ugumu wa kazi unayoifanya huanza kujitokeza.

"Kwani kadri unavyojituma kuwaacha wenzako nao hujitahidi kupunguza tofauti uliyowaacha, hapo ndipo penye kazi ngumu inayohitaji uzoefu na roho ngumu," anasema.

"Siri ya ushindi ni mazoezi, lazima ufanye mazoezi kwa kuangalia malengo ya mbele, riadha ni sehemu ya maisha yangu, inaniingizia kipato na ni ajira yangu. Ndio maana naiheshimu na kuitendea haki," anasema Giniki.

Anaueleza ushindi huo kuwa ni wa Watanzania kutokana na ukweli kwamba alipokuwa akiingia Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, mamia ya watazamaji waliofurika walijawa furaha kwa kumshangilia.

"Kama utakumbuka watazamaji uwanjani walijawa furaha kuona na kwenda kumalizia vizuri mbio na kuiletea sifa nchi, ndio maana nasema ushindi ni wetu Watanzania," anasema Giniki.

Mwanariadha huyo anayezidi kujitangaza kimataifa anawapa ushauri wanariadha nchini kuwa wanapaswa kutanguliza uzalendo na kujituma zaidi ili kuiletea sifa nchi.

"Mara nyingi mashindano haya yanatawaliwa na wanariadha wa nchi jirani, sisi kama wenyeji tunapaswa kujituma na kupiga kifua ili tuonekane tunafanya vizuri," anasema Giniki.

Mashindano hayo ya kilometa 21 yaliyodhaminiwa na Kampuni ya simu za mkononi ya tiGO, ambapo mwanariadha Giniki anawaomba wadhamini hao kujitahidi kuongeza udhamini wao kwa washindi.

Anasema kwa walioshiriki kilometa 42 mbali ya kupewa zawadi za ushiriki bado walipewa zawadi nyingine nje na za ushiriki kama motisha husan kwa wanariadha wa Kitanzania ikiwa ni sehemu ya kuwatia moyo.

"Kwetu haikuwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba tuangalie uwezekano kwa wakati mwingine kuwapa motisha zaidi Watanzania wanaofanya vizuri. Nakiri kuwa tiGO imefanya jambo jema na la kizalendo kudhamini mbio hizi, lakini kwa mtazamo wangu wengine kuongeza nguvu na kuwaunga mkono tiGO," anasema Giniki.

Akifafanua kuhusu mbio hizo kutawaliwa na wanariadha kutoka Kenya, anasema wanariadha wa Tanzania wengi wao huwa hawafanyi mazoezi ya kutosha kabla ya kuingia kwenye mbio jambo linalosababisha wanashindwa kufanya vizuri.

"Mashindano ya Kilimanjaro Marathon ndani yake yakiwa na tiGO Kili Half Marathon ni mashindano makubwa na ambayo pia yana ushindani mkubwa yakihusisha watu kutoka mataifa mbalimbali. Ni muhimu washiriki wa Kitanzania wakalielewa hili na hivyo kujiandaa vizuri wakifahamu kuwa wanashindana na mataifa mbalimbali.

"Kwa upande mwingine, kuna haja ya kuboresha motisha zaidi kwa washiriki wazawa ili kuwapa moyo. Mara nyingi wamekuwa wakikimbilia kushiriki mashindano makubwa wanayoamini wakifanya vizuri watapata kipato angalau kikubwa," anasema Giniki.

Anaitaja sababu nyingine inayosababisha wanariadha wa Kenya kutamba kwenye mashindano hayo ni kutokana na wingi wa washiriki ukilinganisha na washiriki kutoka Tanzania.

"Wanariadha wa Kenya ukiwakuta kwenye mazoezi si chini ya watu 100, hapa kwetu utakuta wanariadha wakifanya mazoezi ni kuanzia wanne, watano hawawezi kuzidi 10.

"Kwa mazingira hayo ukiwakuta wanariadha wa Kenya wakifanya mashindano ya ndani ya kupata nafasi huwa ni mchakato mgumu sana.


"Mashindano ya ndani kwa Kenya ni magumu kupata nafasi kuliko hata mashindano mengine ya dunia. Sasa wingi wa hawa wanariadha wanaokuja kukimbia Tanzania hutokana na wengi wao kukosa nafasi ndani ya nchi.

"Hivyo huamua kutoka nje washiriki mashindano ili wapate nafasi za kujulikana zaidi, lakini pia kurudisha gharama walizotumia kwenye mazoezi," anasema Giniki.

Akizungumzia mbio za tiGO Kili Half Marathon na njia wanayopita anasema, njia hiyo mbali ya kuwa na milima wakati wa kwenda na miteremko wanaporejea bado huwa ni kivutio zaidi kwa washiriki wageni.

"Njia tunayotumia kukimbia kilometa 21, kwa kweli inatangaza vivutio vya utalii wetu kwanza kijiografia, mazingira huwa ni mazuri yanayotangaza utalii," anasema Giniki.

NAJUA WAJUA



Huddersfield imeshuka daraja ikiwa imebakiza mechi sita kumaliza msimu, inajiunga na timu zilizowahi kushuka mapema zaidi kabla ya msimu kumalizika kwenye zama za Premier League (Derby County - 2007-08 na Ipswich Town - 1994-95).

SOKA




Mashujaa wa Yanga dhidi ya Alliance FC, kipa Klaus Kindoki na mfungaji wa bao lao juzi, Heritier Makambo, katika moja ya mechi za timu hiyo. **PICHA: MAKITABA**

# YANGA ILIVYOFUTA JINAMIZI FA CUP NA HOFU KWA LIPULI

**Na Adam Fungmwango**

HATIMAYE timu ya Yanga imefuta jinamizi la msimu uliopita la kutolewa hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama FA Cup, baada ya kuitoa Alliance kwa mikwaju ya penalti 4-3 kwenye mechi kali iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

**Katika mechi hiyo iliyoshuhudiwa Jumamosi iliyopita, kipa raia wa DR Congo, Klaus Kindoki, alikuwa shujaa wa Yanga baada ya kuokoa penalti mbili ikiwamo muhimu ya mwisho iliyopigwa na nahodha wa timu ya Alliance FC, Siraji Juma.**

Dakika 90 za mchezo wa juzi wa hatua hiyo ya robo fainali ulikamilika kwa Alliance kutoshana nguvu na Yanga kwa kufungana bao 1-1.

Yanga walitangulia kufunga bao dakika ya 38 lililofungwa na Heritier Makambo na kwa upande wa Alliance bao lao la kusawazisha katika kipindi cha pili likifungwa na Johnson James.

Baada ya mwamuzi kuamua matuta, Yanga walianza kupiga kupitia kwa beki kisiki Kelvin Yondani ambaye aligongesha kwenye mwamba, Paul Godfery alifunga penalti yake, Thaban Kamusoko alifunga kwa staili ya 'paneka' (kuubetua), Mrisho Ngassa penalti yake iligonga mwamba na Haruna Moshi alifunga penalti kiufundi.

Kwa upande wa Alliance penalti ya kwanza ilifungwa na Joseph John, Martin Kigi aligongesha kwenye mwamba, Dickson Ambundo alikosa, Jofrey Luseke alifunga penalti na Samir Vincent alifunga.

Baada ya kumaliza penalti tano tano kila upande, kwa timu zote matokeo yalisomeka 3-3 baada ya Yanga kukosa penalti mbili na Alliance pia idadi kama hiyo.

Hatua ya kupiga penalti mojamoja ikachukua nafasi na Deus Kaseke alishinda penalti yake na kwa upande wa Alliance, nahodha Siraj Juma shuti lake liliokolewa na Kindoki.

Kwa ushindi huo, Yanga wanatinga hatua ya nusu fainali na kuifuata Lipuli ya Matola kwenye hatua ya nusu fainali ya kwanza na ile ya pili itakuwa kati ya KMC na Azam FC.

**YAVUNJA REKODI YA MWAKA JANA**

Yanga imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali na kuvunja rekodi ya mwaka jana, kwani Aprili Mosi, mwaka jana ilipotolewa kwenye hatua ya robo fainali na Singida United.

Ililazimika kusafiri hadi kwenye Uwanja wa Namfua, na mchezo ulimalizika dakika 90 kwa sare ya 1-1, bao la Yanga likifungwa na Yusuph Mhilu dakika ya 23 na Singida likafungwa na Kenny Kelly dakika ya 83.

Mikwaju ikaamua mshindi na Singida ikashinda kwa penalti 4-2, Emmanuel Martin na Papy Tshishimbi ndio waliokosa penalti kwa upande wa Yanga, matokeo ambayo yaliifanya Singida kwenda kucheza nusu fainali dhidi ya JKT Tanzania na kufungwa fainali dhidi ya Mtibwa Sugar.

**YAWEKA REKODI YA 2017**

Ushindi huo pia umeifanya Yanga kuweka rekodi yake yenyewe ya mwaka 2017 ilipofanikiwa kufika hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA.

Hata hivyo ilikuwa ndiyo mwisho wake, kwani Aprili 30 ilitolewa kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mbao FC lililofungwa na Habib Kyombo na kuifanya timu hiyo kutinga fainali, lakini ilifungwa mabao 2-1 na Simba ambayo ndiyo ilitwaa kombe hilo kwa mwaka huo.

Yanga sasa itavaana na Lipuli ili kuona kama itavunja rekodi ya mwaka 2017 baada ya kuishia hatua hiyo.

Mechi dhidi ya Lipuli inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na hivi karibuni, Yanga kuchapwa bao 1-0 dhidi ya timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabingwa hao wa zamani wanataka kutengeneza rekodi yao nyingine kwani ndiyo timu ya kwanza kutwaa Kombe la FA liliporejeshwa tena baada ya miaka mingi mwaka 2015/16 ilipoichapa Azam FC mabao 3-1 kwenye mechi ya fainali.

Fainali ya mwaka huo inaweza kujirudia kama Yanga itaifunga Lipuli na Azam ikaiondoa KMC kwenye hatua ya nusu fainali.

**ZAHERA HOFU KWA LIPULI**

Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, pamoja na ushindi huo ameweka wazi kuwa hakufurahishwa na kiwango cha timu yake kwenye mchezo huo na kuwasifia Alliance kuwa walikuwa bora zaidi yao.

"Bado tuna kazi kubwa mbele yetu...., tuna mchezo dhidi ya Lipuli kwenye mashindano haya, Lipuli wamekuwa wakitusumbua na mchezo wa mwisho walitufunga, hivyo lazima tujipange vizuri kabla ya kuwakabili," alisema Zahera na kuongeza:

"Kwa mchezo tuliocheza dhidi ya Alliance tuna kazi kubwa kuvuka, ni lazima wachezaji wangu wabadilike na kila mmoja kutimiza majukumu yake angalau kwa asilimia 90."

**NDANI YA UWANJA**



Marcus Rashford na Anthony Martial, wamefunga wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Watford. Hii ina maana ni mara ya kwanza tangu msimu wa 1995-96 (Paul Scholes, Andrew Cole, Ryan Giggs na Eric Cantona) kwa Manchester United kuwa na wachezaji wanne (Martial, Rashford, Romelu Lukaku na Paul Pogba) wote kufunga angalau mabao 10 katika msimu mmoja wa Ligi Kuu England, EPL.

SOKO la uhamisho wa wachezaji limepanda thamani kwa kipindi cha miaka michache. Na imekuwa kama mchezo, kwani mchezaji X akiwa na thamani kubwa basi mchezaji Y atakuwa na thamani kubwa zaidi.
**Uk. 16-17**

# WAKALI 10 DUNIANI WAKUKOKOTA MPIRA




LIONEL MESSI

**MADRID,** Hispania

UKOKOTAJI wa mpira ni moja ya kitu ambacho kinavutia sana katika mechi. Ni sanaa inayowezekana kwa wachezaji wachache tu. Mkokotaji anaweza kuwa anaelekea ana kwa ana mbele ya maadui wawili ama watatu kwa wakati huo na kisha kufanikiwa kutimiza lengo lake, jambo ambalo ni vigumu kulielezea.

Mchezo huu umezalisha wakokotaji wengi. Diego Maradona, Pele, Ronaldinho, Zinedine Zidane, George Best, Johan Cruyff, Garrincha, Ronaldo Nazario, na Roberto Baggio ni miongoni mwa wakokotaji mpira wa wakati wote. Lakini hapa tukiwa tunasubiri orodha mpya ya wakali wa kukokota mpira kwa kipindi cha tangu Januari hadi sasa, hebu tujikumbushe wakali 10 wa kipindi kilichomalizika...

**10. DRIES MERTENS- UKOKOTAJI: 90**

Kiwango cha alama kwa ujumla ni 87. Dries Mertens ni ingizo la kushangaza mbele ya Cristiano Ronaldo. Nyota huyu wa kimataifa wa Ubelgiji ni mmoja wa washambuliaji bora katika soka la Ulaya. Alikuwa mmoja aliyeonyesha kiwango cha juu Serie A kwa misimu miwili iliyopita. Alikamilisha ukokotaji wa mpira kwa takriban wastani wa 1.4 kwa mechi akiwa na Napoli katika mechi 73 zilizopita ambazo alicheza.

**9. PHILIPPE COUTINHO- UKOKOTAJI: 91**

Kiwango cha alama kwa ujumla ni 88. Philippe Coutinho ni mmoja wa viungo bora duniani kwa sasa. Nyota huyu wa kimataifa wa Brazil anajulikana kutokana na uwezo wake kiufundi na akili. Ni sahihi kabisa kuwamo katika orodha hii.

Coutinho alitua Barcelona Januari na amekuwa mchezaji muhimu kwa miamba hiyo ya Catalunya. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, amekamilisha ukokotaji wa mpira kwa kiwango cha wastani wa 2.5 kwa mechi katika misimu miwili iliyopita.

**8. DOUGLAS COSTA- UKOKOTAJI: 91**

Kiwango cha alama kwa ujumla ni 86. Mshambuliaji huyu wa Juventus ni mmoja wa wachezaji wanaotumia akili sana kwenye soka duniani. Nyota huyu wa zamani wa Bayern Munich anamiliki vema mpira kwa akili. Douglas Costa, 28, alikamilisha ukokotaji wa mpira kwa wastani wa 3.4 na 2.5 kwa mechi katika misimu miwili iliyopita wa 2017/18 na 2016/17 kwenye ligi.

**7. LORENZO INSIGNE- UKOKOTAJI: 91**

Kiwango cha alama kwa ujumla ni 88. Ingizo lingine la kushangaza katika orodha hii, Insigne amekuwa katika kiwango kisichotetereka Napoli.

Insigne, 27, amekamilisha ukokotaji kwa takriban wastani wa 1.5 kwa mechi akiwa na Napoli katika mechi 111 zilizopita za Serie A alizocheza. Ingawa ni mshambuliaji mkubwa, Insigne si mzuri sana pindi linapokuja suala la ukokotaji na alama kwa jumla ni 91 zikionekana kidogo.

**6. PAULO DYBALA- UKOKOTAJI: 91**

Alama zake kwa ujumla ni 89. Mchezaji wa nne wa Serie A katika orodha hii. Dybala, 24, alikuwa mshambuliaji bora wa Juventus msimu uliopita akiwa na mabao 22 na pasi za mwisho tano Serie A.

Nyota huyu wa kimataifa wa Argentina amejiendeleza kuwa mshambuliaji wa daraja la juu duniani akiwa Juventus. Dybala alikamilisha ukokotaji wa mpira kwa 2.8 kwa mechi akiitumikia Juventus kwenye Serie A msimu uliopita. Ni mmoja kati wenye kiwango cha juu katika FIFA 19 na amepata alama 91.

**5. LUKA MODRIC- UKOKOTAJI: 91**

Alama kwa ujumla ni 91, mchezaji huyu wa kimataifa wa Croatia anaelezwa kuwa kiungo aliyekamilika zaidi duniani kwa sasa. Luka Modric alibeba majukumu muhimu hivi karibuni wakati Real Madrid ikitwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya na alikuwa muhimu kwa Croatia katika michuano ya Kombe la Dunia Urusi 2018. Ingawa hata hivyo, kiungo huyo mwenye umri wa miaka 33 wastani wake wa ukokotaji mpira ni 1.6 kwa mechi kwenye La Liga kwa misimu mitatu iliyopita, amepewa alama 91.

**4. ISCO- UKOKOTAJI: 92**

Alama kwa ujumla wake ni 89. Nyota huyu wa kimataifa wa Hispania amekuwa mmoja wa wachezaji wa Real Madrid ambao kiwango chao kimesimama vilivyo kwa miaka michache iliyopita. Isco amefunga mabao 17 na kutengeneza mengine 15 kwa 'Los Blancos' hao katika misimu miwili ya hivi karibuni kwenye La Liga akiwa hapo Santiago Bernabeu. Mchezaji huyu mwenye kasi miguuni mwake, ambayo imemwezesha kuwa na wastani wa ukokotaji mpira kwa mechi wa 5.8 katika Kombe la Dunia 2018.

**3. EDEN HAZARD- UKOKOTAJI: 94**

Alama zake kwa ujumla ni 91. Eden Hazard alionyesha kiwango kikubwa Kombe la 2018 akicheza kwa akili kubwa, ambapo aliweza kukokota mpira kwa wastani wa 6.7 kwa mechi katika sita alizocheza, nyota huyu wa Chelsea alikamilisha ukokotaji mpira zaidi katika Kombe la Dunia 2018. Hazard, 27, wastani wake wa ukokotaji mpira ni 4.9 kwa mechi katika msimu wa 2017/18 kwenye Premier League msimu uliopita. Kipindi chake chote kisoka, Hazard amekuwa akipata mafanikio zaidi anapoingia kuchukua nafasi ya mchezaji mwingine.

**2. NEYMAR- UKOKOTAJI: 95**

Kiwango cha alama zake kwa ujumla ni 92. Mbrazil huyu ni mmoja kati ya washambuliaji wakali zaidi duniani kwa sasa. Mchezaji aliyejaliwa mbinu kiufundi, Neymar anachukuliwa kama mchezaji anayetumia akali sana.

Neymar, 26, amekamilisha ukokotaji wa mpira kwa wastani wa 7.1 kwa mechi katika mashindano yote msimu uliopita akiwa na Paris Saint-Germain. Hata akiwa na Barcelona, Neymar alikamilisha ukokotaji kwa wastani wa 5 kwa mechi katika misimu yake miwili ya mwisho Camp Nou.


**1. LIONEL MESSI - UKOKOTAJI: 96**

Alama alizopata kwa ujumla ni 94. Lionel Messi ndiye anayeshika namba moja. Mmoja wa wachezaji bora zaidi katika soka wa wakati wote, kama si yeye bora zaidi, Messi amekuwa maarufu sana sana kwa Barcelona.

Messi, 31, amekamilisha ukokotaji wa mpira kwa wastani wa 4.6 kwa mechi katika misimu 10 ya La Liga iliyopita. Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina pia ana rekodi kubwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Takwimu hizo ni hadi Septemba mwaka jana.

## USILOLIJUA



TANGU alipoichezea Manchester United kwa mara ya kwanza Februari 2016, Marcus Rashford ameifungia mabao 45 katika mashindano yote, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote katika klabu hiyo.



## CCM yaingilia kati mgogoro wa ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimeiagiza Serikali ya Mkoa huo, kumaliza mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Mtaa wa Sae na Chuo cha Kilimo cha Uyole jijini Mbeya, ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Katibu wa CCM wa Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda, alipofanya ziara ya kutembelea eneo hilo na kusikiliza kero za wananchi wa eneo hilo ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia kuporwa eneo hilo.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kinachoongozwa na Mwenyekiti wake Rais Dk. John Magufuli, kitahakikisha mgogoro huo unaisha ndani ya miezi miwili ili wananchi waendelee kujenga, kulima na kulitumia eneo hilo kwa shughuli za kufyatua tofali.

Alisema baada ya kupokea barua ya malalamiko kutoka kwa wananchi hao, alifuatilia na kukuta baadhi ya barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya ambazo zinamshauri Mkuu wa Mkoa namna ya kutatua mgogoro huo.

"Tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, sisi kama chama tunauhitaji mtaa huu, tunaihitaji kata hii na tunalihitaji jimbo hili, sasa kama mgogoro huu umedumu miaka 30 basi utaisha ndani ya miezi miwili na tutamwagiza Mkuu wa Mkoa aushughulikie haraka," alisema Itunda.

Aliwataka wananchi hao kuendelea kuvuta subira wakati Serikali ya Mkoa ikiendelea kuutatua mgogoro huo na chama kitaendelea kusimamia.

Awali baadhi ya wananchi wa mtaa huo pamoja na viongozi wa mila, walimweleza katibu huyo changamoto zinazowakabili kutokana na mgogoro huo.

Mwenyekiti wa machifu wa Mkoa wa Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, alisema kilio cha wananchi hao ni cha muda mrefu na kwamba baadhi ya waathirika walishafariki na kuacha mgogoro huo ukiendelea kutokota.

# Waziri atoa siku 28 umeme kuwashwa kata 2

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametoa siku 28 kwa Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (Rea) kwa kushirikiana na Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kujenga na kukamilisha njia ya umeme yenye urefu wa zaidi ya kilometa 20 pamoja na kuhakikisha umeme unawashwa kwenye makazi ya wananchi katika kata mbili wilayani Kyela.

Waziri Kalemani alitoa agizo hilo jana, wakati akizungumza na wananchi katika Kata ya Ipande ambako alistushwa baada ya kuelezwa na wananchi kuwa Kata za Nkokwa na Ipande hazijawahi kufikiwa na umeme hata kwenye kijiji kimoja tangu serikali ilipoanza mpango wa kusambaza umeme vijijini na kukusudia kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini.

Alisema haiwezekani kata nzima za Ipande na Nkokwa ziwe hazijafikiriwa kupelekewa umeme kwa kipindi chote tangu serikali ilipoazimia kupeleka umeme katika vijiji vyote na kwamba kitendo hicho kinaonyesha kuna mahali uzembe unafanyika miongoni mwa watekelezaji wa mpango huo.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Kalemani aliiagiza Rea kwa kushirikiana na Tanesco kuanza mara moja kazi ya kuchimbia nguzo kuelekea kwenye kata hiyo na kutoa mwezi mmoja kazi hiyo kuwa imekamilika na umeme uwashwe kwenye makazi ya wananchi.

"Naagiza kazi ianze leo na kufikia tarehe 28, Aprili umeme uwashwe kwenye kata hizi za Nkokwa na Ipande, ikiwa agizo hili halitatekelezwa nawaambieni watendaji wangu wa Rea na Tanesco mtapungua au kumalizika kabisa kwenye nafasi zenu," alisema Dk. Kalemani.

Alisema suala la usambazaji wa umeme vijijini sio la hiari kutokana na serikali kuazimia vijiji vyote nchini vifikiwe na umeme na kila mwananchi apewe fursa ya kuingiza kwenye nyumba yake.

Hata hivyo, wakati Dk. Kalemani akitoa agizo hilo, Mbunge wa Kyela ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema Aprili 28, kutakuwa na tukio kubwa la kitaifa, hivyo akamwomba awaongeze watendaji wake japo siku tatu mbele.

"Mheshimiwa Waziri, tarehe 28, Aprili timu yetu ya vijana wenye umri wa chini ya miaka 17, Serengeti Boys watakuwa uwanjani wakiwania taji la Afrika, hivyo naamini Watanzania wote watakuwa wakifuatilia mchezo huo, nakuomba usogeze mbele japo kwa siku tatu ili na hawa watendaji nao wapate fursa ya kuiangalia timu yetu ikiwa uwanjani," alisema Dk. Mwakyembe.

Ambi hilo lilikubaliwa na Dk. Kalemani ambaye alikubali kusogeza mbele hadi Mei 2 na kuahidi kurejea tena wilayani Kyela kwenda kukagua utekelezaji wa mradi huo.

Akiwa wilayani Kyela, Waziri Dk. Kalemani pia alitembelea na kuwasha umeme katika vijiji vya Makwale na Ibale katika Kata ya Makwale pamoja na kuwasha umeme katika Shule ya Msingi Mapinduzi, iliyopo kata ya Mababu na baadaye kuzungumza na wananchi katika mji mdogo wa Ipinda wilayani Kyela.

Akizungumza na wananchi wa Ipinda, Waziri Dk. Kalemani alipiga marufuku tabia ya Shirika la Umeme kupandisha bei ya kuunganishia wananchi umeme majumbani baada ya kukabidhiwa miradi ya Rea vijijini.

Alisema amegundua kuwa Tanesco wakishakabidhiwa miradi hiyo, hupandisha bei ya kuunganishia umeme wananchi majumbani kutoka Sh. 27,000 hadi Sh. 177,000 jambo ambalo alilosema ni kinyume na maagizo ya serikali.

"Bei ya kuunganisha umeme majumbani, vijijini nchi nzima ni shilingi 27,000 tu, bei hii ndiyo iliyotolewa na serikali bila kujali mwananchi wa kijijini anapewa umeme huo na Rea au Tanesco, hivyo kuanzia leo ni marufuku kupandisha bei ya kuunganisha umeme vijijini na wananchi wote watalipa shilingi 27,000 tu," alisisitiza Dk. Kalemani.

Wilaya ya Kyela bado inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na hadi sasa zaidi ya vijiji 41 bado havijapata nishati hiyo.



Baadhi ya vijana waendesha pikipiki maarufu kwa jina la Boda boda wa Jiji la Mbeya wakiongoza maandamano wakati wa maadhimisho ya siku ya Kifua Kikuu mkoani Mbeya ambayo yalifanyika katika Kituo cha Daladala cha Kabwe. **PICHA : NEBART**

# Mbeya yatajwa ongezeko ugonjwa kifua kikuu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umetajwa kuwa miongoni mwa mikoa 10 nchini inayokabiliwa na ongezeko kubwa la watu wenye maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu na kuanzia mwezi Januari mpaka Desemba 2018 wagonjwa 3,325.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyata, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani ambayo kimkoa yaliandaliwa na Kituo cha Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (MMRP) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya.

Dk. Manyata alisema idadi hiyo ya wagonjwa ni asilimia 69 ya lengo ambalo serikali iliupa mkoa ambalo ilikuwa kuibua wagonjwa 4,835 na kusema wataendelea na juhudi za kuwaibua na kuwapatia tiba wagonjwa ili kuhakikisha ugonjwa huo unatokomea.

Alisema wagonjwa hao walikuwa wanaibuliwa majumbani na katika vituo mbalimbali vya afya ambavyo vinapima ugonjwa huo na kwamba asilimia 14 pekee ndio waliibuliwa majumbani.


Hata hivyo, alisema asilimia 69 ya wagonjwa wa kifua kikuu waliobuliwa mkoani humo walibainika kuwa wanaishi pia na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU), hivyo akasisitiza kuwa magonjwa hayo huwa yanakuwa kama watoto pacha.

"Utafiti unaonyesha kuwa mtu mwenye kifua kikuu asipotibiwa na akaendelea kuishi nyumbani, anaweza kuambukiza mpaka watu 20, maana huu ugonjwa unaambukizwa kwa njia ya hewa, kwa mkoa wetu utafiti unaonyesha tumewaibua na kuwatibu wagonjwa kwa asilimia 40 pekee na asilimia 60 bado wapo majumbani wanaendelea kuwaambukiza wengine," alisema Dk. Manyata.

Alisema wataendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya mkoani humo kutoa elimu na kuwaibua wagonjwa waliobaki mitaani ili watibiwe na kuutokomeza ugonjwa huo ambao unatibika.

Kwa upande wake Mratibu wa Kifua Kikuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Bonny Ferdinand, alisema katika jiji hilo pekee, wagonjwa wa kifua kikuu wameongezeka kutoka 767 mwaka 2015 mpaka wagonjwa 895 mwaka 2018.

Hata hivyo, alisema baadhi ya wagonjwa walioibuliwa wametibiwa na wameshapona, lakini bado kuna changamoto ya watu kuogopa kujitokeza kwenye vituo vya afya kwenda kupima.





# Elimu kuhusu sikoseli yahitajika

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa Tanzania inashika nafasi ya nne duniani kwa kuwa na wagonjwa wengi wa sikoseli.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Elias Munda, aliyasema hayo wakati wa akizindua Kampeni ya Elimu ya Ugonjwa wa Sikoseli Shuleni jijini hapa jana.

Alisema ili kukabiliana na ugonjwa huo, elimu inatakiwa kutolewa kwa wananchi ili idadi ya watoto wanaozaliwa na ugonjwa huo ipungue.

Alizitaja nchi zingine duniani zinazoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa sikoseli kuwa ni Nigeria, Congo na India.

Hata hivyo, alisema kutokana na idadi ya watu wanaougua ugonjwa huo kuongezeka duniani, shirika hilo litatoa msaada ili kufanya utafiti zaidi wa namna ya kuzuia ugonjwa huo kwa nchi zenye idadi kubwa ya wagonjwa.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia saba ya vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano duniani, inasababishwa na ugonjwa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Asasi na Taasisi zinazojihusisha na ugonjwa wa sikoseli nchini, Dk. Deogratias Soka, alisema mwaka huu wameamua kufanya kampeni hiyo kwa shule za sekondari kwa kuwa wanafunzi ni wazazi watarajiwa.

Dk. Soka alisema kuwa katika kampeni hiyo inayoitwa 'Vunja Mduara wa Sikoseli Shuleni', watatoa elimu kwa wanafunzi na kuwapima kubaini wenye vinasaba vya ugonjwa huo ili kuwapa ushauri na matibabu kwa kuwa dawa zipo.

Alisema wanafunzi ni wazazi watarajiwa, wakipima na kujitambua kama wana vinasaba vya ugonjwa huo, itawasaidia kipindi watakapohitaji kupata familia kuepuka kupata watoto na mtu mwenye vinasaba vya ugonjwa huo.

Dk. Soka alisema mwaka jana walifanya kampeni hizo katika baadhi ya maeneo yakiwamo makanisa, misikiti na shule.

"Dalili za sikoseli ni maumivu makali mwilini yakiambatana na homa kali na kwa watoto waliozaliwa na ugonjwa huo, hulia sana kutokana na maumivu hayo makali wanayoyopata," alisema.

Alibainisha kuwa kati ya watoto 8,000 hadi 11,000, huzaliwa wakiwa na ugonjwa huo kila mwaka na asilimia 70 ya watoto hao kupoteza maisha kutokana na kutopata huduma mapema.

Akizindua kampeni hiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Afya katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Kapologwe Ntuli kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi, Selemani Jafo, alisema serikali inatambua uwapo wa ugonjwa huo na athari zake.

# Wasabato kuchangamkia fursa uwekezaji Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAUMINI wa Kanisa la Waadventista Wasabato wametakiwa kuchangamkia fursa ya ujio wa serikali Dodoma, kuwekeza kwenye sekta mbalimbali zikiwamo afya na elimu ili kujikwamua kiuchumi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Jimbo la Kusini mwa Tanzania wa kanisa hilo, Mch. Walwa Malekana, alipozungumza na waumini wa kanisa hilo Kizota jijini Dodoma.

Alisema kwa sasa Dodoma kuna fursa nyingi, hivyo si vyema waumini hao wakaridhika na kiwango cha uchumi walichonacho na kuwaacha watu kutoka nje ya Dodoma kuwekeza. Aliwataka waumini kufanya uwekezaji wenye tija na kwa wale wenye biashara zao wahakikishe wanaziboresha ili ziwe kubwa kulingana na hadhi ya jiji hilo jipya.

"Si mpango wa Mungu kukaa mahali pamoja kwenye ustawi, kuridhika na hali fulani ya maisha, si mpango wa Mungu," alisema.

Mch. Malekana aliongeza: "Mungu kwenye Kumbukumbu la Torati anawaambia mmekaa Seiri kwa miaka mingi yatosha, kuna watu kwenye maisha haya wameridhika kukaa eneo fulani katika maisha ya kiroho, kiuchumi na hata kujiendeleza kielimu, wameridhika wakati siyo mpango wa Mungu, usiridhike na kiwango cha elimu ulichofikia ukadhani umefanikiwa, huko ni kukaa Seiri.

"Kukaa katika hali fulani ni sawa na kuzunguka Seiri, usiridhike na aina ya utendaji ulionao, lazima upige hatua, wala msiridhike na mambo mliyonayo Waadventista wa Dodoma muone fursa zilizopo nchini, kuna mahitaji nchi inapohamia, wageni wengi watakuja hapa kuna fursa ya nyumba za wageni. "Kuna fursa kama kanisa kupenya kupeleka injili, lakini kuna fursa ya kuwekeza kwenye elimu. Ukiridhika na mambo madogo duniani ni kuzunguka milima ya Seiri.

"Njia aliyoichagua Mungu kusafiri wana wa Israel haikuwa njia rahisi, Mungu anachagua mazingira magumu kwa sababu mbili ili atukuzwe, lakini pia yakukuze kiakili na kiroho.

"Kwa hiyo, kuna watu wanapenda vitu rahisi rahisi maishani, hata wakienda shule wanachagua masomo rahisi yasiyofikirisha."

Mch. Malekana alisema duniani watu wanafeli kwa kuchagua vitu rahisi, huku akitolea mfano wanafunzi kukimbia masomo ya sayansi wakidhani kuwa ni magumu.

"Nawatia moyo wanafunzi kuacha kuogopa masomo ya sayansi wanayodhani ni magumu kwa kuwa ndiyo yatakayoleta maendeleo ya kiuchumi, masomo ambayo wamekuwa wakiyakimbia Mungu hutukuzwa kwa kile unachodhani ni kigumu, maana utakapofaulu utampa Mungu utukufu na kukuza akili yako," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Dodoma (CHAVITA), Yusuph Mloli, akiwashukuru wanachama wake baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Wananchi waomba matuta barabarani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Wilaya ya Chamwino wanaoishi kandokando ya Barabara Kuu ya Dodoma-Morogoro, wameuomba Wakala wa Barabara (Tanroads) kuweka alama na matuta barabarani ili kupunguza ajali zinazotokana na madereva kuendesha kwa mwendokasi.

Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walidai barabara hiyo imekuwa na ajali za mara kwa mara hususan dhidi ya watembea kwa miguu wanapovuka barabara.

Walidai kuna haja kuwekwa alama za kivuko kwenye eneo la Buigiri kutokana na barabara hiyo kuwa jirani na shule ya wanafunzi wenye uoni hafifu na kituo cha watu wazima wenye ulemavu wa macho.

Yared Cheleso, Mwenyekiti wa Kituo cha Wasioona cha Matembe Bora kilichoko Buigiri, alidai madereva wanaotumia barabara hiyo hawazingatii sheria wala alama zilizoko na wanaendesha kwa mwendokasi na kusababishia vifo na ulemavu.

"Cha kusikitisha, madereva hao wanaposababisha ajali hizo za kugonga mtu, hawasimami wala hakuna taarifa yoyote ya kupatikana kwa magari hayo," alidai.

"Tunauomba Wakala wa Barabara kutuwekea alama ikiwa pamoja na matuta ili kupungua ajali hizi ambazo zinapoteza nguvu kazi ya taifa."


Mkazi wa Kijiji cha Chinangali, Magreth Mazengo, aliwaomba askari wa usalama barabarani kwenye barabara hiyo kuhakikisha wanawabaini madereva wanaoendesha magari kwa mwendokasi na kusababisha vifo na ulemavu.

"Tunakiomba Kikosi cha Polisi Barabarani kuimarisha ulinzi wake hasa kuanzia saa 12 jioni hadi asubuhi, hii ni kutokana na ajali nyingi hutokea muda huo ambao madereva wa magari wamekuwa wakitumia kuendesha kwa kasi kwa kuwa askari wanakuwa hawapo barabarani muda huo," alidai.

Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, alisema wananchi wake wameshatoa malalamiko mara kadhaa kuhusu ajali hizo, lakini hakuna taarifa yoyote ya kukamatwa madereva ambao wamekuwa wakigonga watu na kukimbia.

"Ni kweli kwenye vijiji vyangu vilivyoko Kata ya Buigiri madereva wa magari wanaotumia hii barabara ya Dodoma-Morogoro wamekuwa wakiendesha kwa mwendokasi unaosababisha ajali na watu kupoteza maisha yao," alidai.

Yindi aliunga mkono ombi la wananchi hao kuwekwa alama pamoja na askari kuwapo barabarani hadi usiku kwa muda huo madereva wamekuwa wakitumia mwanya wa kutokuwapo kwa askari, kukimbiza magari yao bila kuzingatia sheria.





Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kushoto), akikagua makontena yenye vifaa vipya vya mradi wa REA wilayani Muheza, jana. Wengine ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanasha Tumbo (wapili kushoto) na kulia Mbunge wa Muheza, Adadi Rajabu. **POCHA: STEVEN WILLIAM**

# Shein aiagiza Kamisheni ya Utalii kutoa elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Kamisheni ya Utalii Zanzibar kutoa elimu ya historia ya utalii wa Zanzibar ili kuujua unakotoka na unakokwenda na hatua zilizofikiwa katika kuimarisha uchumi wa nchi.

Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu Mjini Zanzibar alipokutana na uongozi wa Wizara ya Habari, Utalii, na Mambo ya Kale. Alisema kuwa kuijua historia ya utalii Zanzibar kutasaidia kwa kiasi kikubwa kujua na kufahamu lengo lililokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuelewa jinsi utalii ulivyokuwa hapo siku za nyuma na jinsi uliyo hivi sasa na hatua na mafanikio yaliofikiwa kutokana na sekta hiyo.

Dk. Shein alisema kuwa sekta ya utalii imekuja baada ya zao la karafuu kushuka thamani yake na ndipo marehemu mzee Aboud Jumbe Mwinyi akaona haja ya kuimarisha sekta hiyo pamoja na baadhi ya mazao mengine ya viungo.

Alieleza kuwa tokea kipindi hicho sekta ya utalii imeimarika kwa kiasi kikubwa kwa kuwapo vivutio kadhaa hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar inajitangaza yenyewe kutokana na vivutio vilivyopo.

Alisema kuwa hivi sasa Zanzibar iko vizuri kiutalii ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo siku za nyuma kwa kuwa utalii wa Zanzibar unasifika zaidi duniani kote na kufanya watalii wengi kuja kuitembelea Zanzibar.

"Hivi sasa utalii wa Zanzibar unaongozwa na sheria ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2012 kwa lengo la kuufanya utalii uwe kwa wote kwa kuwa ndio uchumi wa Zanzibar," alisema.

Alieleza kuwa sheria ndio ngao kubwa ya kuendesha kamisheni ya utalii, hivyo alisisitiza kamisheni pamoja na makamishna wote kuizingatia na kuifanyia kazi sheria hiyo pamoja na kanuni zake ili iweze kuwasaidia kuendeleza sekta hiyo.

Aidha, Dk. Shein alieleza maamuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa sekta zote zinabebwa na sekta ya utalii pamoja na kuonyesha umakini wake katika sekta hiyo na kuipa dhamana kamisheni hiyo.

Naye Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Idd, alisema sekta ya utalii ni muhimu katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar na kukuza pato la taifa, hivyo kuna haja ya sekta hiyo kuimarishwa.

Aidha, Balozi Iddi alieleza haja ya kujifunza katika kuiendeleza sekta hiyo hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ina vivutio vingi pamoja na historia katika mambo ya utalii ikilinganishwa na visiwa vyengine vikiwamo vile vilivyopo katika Bahari ya Hindi ambavyo vimejitangaza vyema na kupokea wageni wengi.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alieleza jinsi Zanzibar ilivyopata mafanikio katika sekta ya utalii na jinsi wawekezaji na wageni wanaofika kuwekeza na kuitembelea Zanzibar.

Alisema wizara yake imeweka mikakati katika kuhakikisha idadi ya watalii inaendana na mapato yanayopatikana kutoka katika sekta hiyo.

# Mkoa wa Magharibi wapania kuongeza ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema ajenda ya maendeleo katika mkoa huo ni kukuza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Akizungumnza baada ya kupokea ripoti ya kamati maalum ya maendeleo ya elimu ya mkoa huo, alisema ameridhishwa na kiwango cha ufaulu cha matokeo ya kidato cha nne mwaka 2018 kwa mkoa huo.

Alisema kiwango hicho kimetokana na juhudi za walimu, wanafunzi, wazazi na uongozi wa mkoa huo katika kuhamasisha suala la elimu na kuwaandalia mazingira mazuri ya kupata elimu watahiniwa ndani ya mkoa huo.

Alisema miaka mitatu iliyopita mkoa huo ulikuwa na wimbi kubwa la kufeli kwa wanafunzi, hali iliyosababisha kuundwa kwa kamati maalum ya elimu ambayo kwa kiasi imeanza kuzaa matunda.

"Miaka mitatu iliyopita Mkoa wa Mjini Magharib Unguja tulikuwa ni miongoni tunaotoa shule za mwisho zilizofanya vibaya katika mitihani ya kidato cha nne, lakini kwa sasa tumepiga hatua na kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka 2018 hatukuwamo katika orodha hiyo," alisema.

Aidha, alieleza kuwa mikakati ya mkoa wake ni kuondosha zero kwa mitihani yote ya kidato cha nne na la sita ili mkoa huo uweze kutoa wataalamu watakaoweza kuisaidia nchi yao.

Ayoub aliwataka wanafunzi wa kidato cha nne na sita kusoma kwa bidii kwa kuwa wanakabiliwa na mitihani yao ya taifa mwaka huu na kuwaahidi kuwa kwa atakayefanya vizuri atawazawadia zawadi mbalimbali.

Alisema atazinunua alama zote za ufaulu wa daraja la kwanza kwa matokeo ya kidato cha nne ambayo yametangaziwa mwaka huu na Baraza la Mitihani ya Taifa.

"Kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka 2018, mkoa wangu umetoa alama za ufaulu wa daraja la kwanza ambazo ni 147 na hizi nitazinunua kwa kila moja shilingi laki moja na fedha hizo nusu zitakwenda kwa wanafunzi waliopata alama hizo na nusu zitakwenda kwa walimu ambao nao wanamchango mkubwa," alisema.

Akiwasilisha ripoti maalum ya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa huo, Mwenyekiti Juma Abdallah, alisema kuwa katika Mkoa huo umekuwa na ufaulu wa daraja la kwanza 147 katika matokeo ya mtihani ya kidato cha nne mwaka 2018, idadi ambayo ni kubwa ikilishanganishwa na mwaka 2017, ambao wafaulu walikuwa 106 katika daraja hilo.

Aidha, alisema ufaulu wa daraja la pili katika matokeo hayo ni 638 na daraja la tatu ni 1,341 ambapo pia umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017.

# Jang'ombe watakiwa kuweka mazingira safi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wa Jimbo la Jang'ombe wametakiwa kufanya usafi wa mazingira mara kwa mara ili kuepuka madhara yanayosababishwa na uchafu yakiwamo maradhi ya miripuko.

Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Ramadhan Hamza Chande, aliyasema hayo katika shughuli ya kufanya usafi katika hospitali ya wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu.

Alisema kila mwananchi ana jukumu la kufanya usafi katika mazingira anayoishi kwa kuhakikisha yanakuwa safi muda wote kwa lengo la kuepuka maradhi yakiwamo ya kipundupindu, kichocho na malaria.

Alisema lengo la kufanya usafi katika eneo la hospitali ni kutoa msaada wa kijamii wa kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum ambao ni wagonjwa wa akili wanaohitaji huduma muhimu za kijamii zikiwamo kuishi salama na katika mazingira safi.

Alisema zoezi hilo la usafi ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020, iliyoainisha utekelezwaji wa mambo mbalimbali katika sekta ya afya ikiwamo usafi na ulinzi wa mazingira.

Mwakilishi huyo alieleza kwamba ufanyaji usafi utakuwa endelevu na kutekelezwa kwa kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha wananchi wafanye usafi kwa hiari.

"Naomba wananchi watambue na kuamini kuwa usafi ni tabia hivyo tunatakiwa kuweka safi mazingira yetu na yale wanayoishi watu wenye mahitaji maalum ili nao waishi kwa amani, utulivu na usalama wa afya zao kama wanavyoishi watu wengine," alisema.

Aidha, aliishauri serikali kupitia Baraza la Manispaa la Mjini kuhakikisha wanasimamia sheria ndogo ndogo za ulinzi wa usafi wa mazingira ili watu wanaochafua mazingira watozwe faini za papo kwa papo kwa lengo la kubadilisha jamii kitabia na kutambua umuhimu wa kulinda mazingira.

Akizungumza wakati wa ufanyaji usafi, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini Said Juma Ahmada, alisema baraza hilo linasimamia shughuli za usafi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha mji unakuwa safi na unaoendana na hadhi ya Zanzibar.

Alisema wananchi wanatakiwa kuheshimu sheria za manispaa kwa kuhakikisha maeneo ya mji yanakuwa safi muda wote ili kurejesha sifa ya Zanzibar ya kuwa mji safi na wenye watu wastaarabu katika kulinda na kutunza mazingira yaliyowazunguka. Alieleza kwamba lengo la manispaa hiyo ni kufikia kiwango cha Mji wa Zanzibar kutajwa katika miji safi, kimataifa, kikanda na kitaifa kama inavyotajwa mji wa Arusha na Mwanza kwa Tanzania Bara.

Kwa upande wake Katibu wa Hospitali ya Kidongo Chekundu, Bhai Ibrahim, aliwashukuru wadau walioshiriki na kutoa msaada wa vifaa vya usafi.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 29 March**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

# Trump atishia kufunga mpaka wa Marekani na Mexico

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametishia kufunga mpaka wa Marekani na Mexico, endapo Mexico hawatachukua hatua madhubuti za kuwazuia wahamiaji kuingia nchini Marekani.

Hatua hiyo ya kufunga mpaka inatishia kupoteza biashara yenye thamani ya mabilioni ya dola za kimarekani.

Tishio hilo limekuja baada ya kuwapo kwa wimbi kubwa la wahamiaji wanaoingia Marekani wakitokea Mexico kwa nia ya kutafuta hifadhi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Marcelo Ebrard, kwenye ukurasa wake wa Twitter aliandika kuwa: "Mexico ni jirani mzuri kwa Marekani, lakini haitachukua hatua kutokana na vitisho."

Rais Trump aliwaambia wanahabari siku ya Ijumaa kuwa kuna uwezekano mkubwa akafunga mpaka wiki ijayo.

Alisema ni rahisi sana kwa Mexico kuzuia wahamiaji haramu kuingia Marekani, lakini hawajaamua kufanya hivyo.

Rais Trump hivi karibuni aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter ambapo alihitimisha kwa kusema kuwa: "Marekani inapoteza pesa nyingi kwa ajili ya wahamiaji, hasa unaposhughulikia suala la uingizaji wa dawa za kulevya nakadhalika, kufunga mpaka litakuwa jambo jema."

**MEXICO INASEMAJE?**

Rais wa Mexico, López Obrador, alisema kuwa suala la wahamiaji siyo la raia wa Mexico.



Alisema tatizo hilo limeota mizizi katika eneo la nchi za Amerika ya kati zaidi kuliko Mexico.

"Raia wa Mexico hawatafuti tena kazi nchini Marekani. Wengi wa wahamiaji wana asili ya nchi za Amerika ya Kati," alisema Obrador.

Kutokana na kauli ya Trump, Rais Lopez aliuambia mkutano kuwa: "Ninataka kuweka wazi kuwa hatutagombana na serikali ya Marekani, bali tutazidisha upendo na amani."

Alizungumzia kuhusu uhamiaji, Rais Trump alisema: "Ni haki ya mwanadamu, watu wa America ya Kati hawana namna ya kufanya hivyo hutafuta namna ya kupata maisha bora."

**SABABU TRUMP KUFUNGA MPAKA**

Vyombo vya usalama vilifanya doria na vimekuwa vikishuhudia idadi kubwa ya watu wanaotafuta hifadhi wakikimbia machafuko katika miji ya El Salvador, Honduras na Guatemala.

Ahadi ya kujenga ukuta bado haijatimizwa kwa kuwa Baraza la Congress lilikataa kuunga mkono, hata hivyo Rais Trump alitangaza hali ya dharura ili apeleke fedha kwenye ujenzi wa ukuta. **BBC**

# Uingereza kujitoa EU bila ya makubaliano

**LONDON,** Uingereza

WABUNGE wa Uingereza wamekataa makubaliano ya nchi yao kujitoa Umoja wa Ulaya 'Brexit', kwa mara ya tatu, ikiwa ni pigo kwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Theresa May.

Gazeti la Telegraph la nchini humo, liliripoti kuwa May anapaswa kujiuzulu mara moja baada ya kufanya majadiliano ya kurefusha uanachama wa muda wa Uingereza katika EU.

"Hapaswi kuona ama kuambiwa wakati anaweza kukutana na Umoja wa Ulaya kujadili kurefushwa kwa Brexit, ni kitu cha kawaida kwamba ndio amefika mwisho wa barabara, ni lazima ajiondoe kwa ajili ya Brexit kwa chama chake na demokrasia," liliandika gazeti hilo katika tahariri yake.

Gazeti la Telegraph limekuwa likipendwa na wanachama wa chama cha May cha Conservative.

**Uwezekano wa May kuanzisha uchaguzi na kuondoa kundi la wabunge wa chama chake cha Conservative kupata wabunge wengi watakaofidia theluthi ya wabunge wote bungeni ni kichekesho.**

Hata hivyo, uwezekano wa kuwa na Waziri Mkuu mpya kuongoza awamu ijayo ya majadiliano ya Brexit ilikuwa haitoshi kuweza kuwavutia wabunge kwenye kikao kilichofanyika juzi.

Baadhi ya wabunge walihofia makubaliano ya May yataiacha Uingereza ikifungwa katika EU iwapo mazungumzo ya baadaye ya biashara yakivunjika.

Kwenye kikao hicho, May, ambaye amenusurika kung'olewa madarakani Desemba mwaka jana, alisema kuwa wangehitaji kuitisha uchaguzi mkuu wa taifa kuweza kupata wingi wa wabunge kwa ajili ya kupitisha sheria ya Brexit.

"Uwezekano wa May kuanzisha uchaguzi na kuondoa kundi la wabunge wa chama chake cha Conservative kupata wabunge wengi watakaofidia theluthi ya wabunge wote bungeni ni kichekesho," lilieleza gazeti hilo.

Gazeti lingine lenye wasomi wengi nchini Uingereza la The Sun lilimtaka May kujiuzulu katika taarifa yake ya ukurasa wa mbele katika toleo lake la Jumatatu.

Gazeti la Daily Mail ambalo linaunga mkono Brexit katika ukurasa wake wa mbele limeuelezea uamuzi wa bunge kupiga kura dhidi ya mipango ya May kuwa ni usaliti kwa Brexit. Rais wa Halmashauri ya EU, Donald Tusk, alisema viongozi wa EU watakutana Aprili 10 kujadili kuondoka kwa Uingereza kutoka kundi hilo la mataifa.

Viongozi kadhaa wa Ulaya wameeleza kuwa Uingereza itajiondoa EU bila ya kupata makubaliano, hali ambayo kampuni zinahofia kutasababisha mtafaruku wa uchumi kwa nchi hiyo. **DW**



Jeshi la Israel likitumia maji kuwatawanya waandamanaji wa Palestina katika ukanda wa Gaza. **PICHA: REUTERS**

# Idadi waliojeruhiwa kwenye maandamano Gaza yaongezeka

**JERUSALEM,** Israel

MAELFU ya wakazi wa mji wa Gaza wameandamana katika mpaka wa Israel kuadhimisha mwaka mmoja tangu kuzuka maandamano na machafuko katika ukanda huo.

Katika maandamano hayo, raia mmoja wa Palestina aliuawa na wengine 13 wakajeruhiwa kwa risasi za moto, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na maofisa wa matibabu wa Kipalestina.

Kundi la Hamas ambalo ndilo linalotawala Ukanda wa Gaza liliahidi kuwaweka waandamanaji mbali na uzio, wakati wajumbe wa Misri wakijaribu kufanikisha makubaliano ya kusitisha mapigano.

Lakini, baadhi ya waandamanaji waliukaribia ukuta huo na kupeperusha bendera za Kipalestina na kurusha mawe na milipuko kuelekea upande wa wanajeshi wa Israeli waliokuwa wameweka ulinzi.

Wanajeshi wa Israel walijibu kwa kufyatua mabomu ya kutoa machozi ili kuwatawanya waandamanaji hao.

Wizara ya Afya ya Gaza ilisema mtu mmoja mwenye umri wa miaka 17 alifariki dunia baada ya kupigwa risasi usoni.

Maandamano hayo yamekuja wakati Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, anawania uongozi katika muhula wake wa nne mfululizo madarakani katika uchaguzi utakaofanyika Aprili 9.

Lakini, Netanyahu anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa kundi la wakuu wa zamani wa jeshi ambao wanaikosoa kile wanachosema ni kushindwa kwa sera yake ya Gaza.

Katika hatua za mwisho za kampeni yake, Netanyahu anahitaji kuleta utulivu katika mpaka wa Israel na Gaza, bila kuonekana kusalimu amri kwa kundi la Hamas.

Netanyahu alikosolewa vikali kwa kile kilichoonekana kuwa ni msimamo dhaifu dhidi ya mashambulizi mapya ya ndege kutokea Gaza.

Hamas kwa upande wao, wanakabiliwa na ongezeko la vurugu katika Ukanda wa Gaza kutokana na kuzorota kwa mazingira baada ya zaidi ya muongo mmoja kufungwa kwa mpaka wa Israel na Palestina. **DW**

# EAC yahimizwa huduma afya kidigitali

**Na Devota Mwachang'a**

NCHI wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimetakiwa kuharakisha mchakato wa kuendeleza kutumia njia mpya ya huduma za afya kidigitali na matumizi ya utafiti wa kisayansi ambayo itasaidia namna ya udhibiti wa magonjwa ya maambukizo kwenye mipaka.

Mapendekezo hayo yalitolewa wakati wa kufungwa kwa mkutano wa saba wa wanasayansi na watoa huduma za Afya ulioshirikisha wataalamu hao kutoka nchi wanachama wa EAC uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Akifunga mkutano huo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema EAC inapaswa kupanua upatikanaji wa dawa, chanjo na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya kidigitali na ili kuboresha upatikanaji na ubora wa habari na huduma za afya.

"Mkutano huu ni wa mafanikio na tumetoa mapendekezo ambayo yanatupa njia ya wazi, na kujitolea juu ya afya ya kidigitali. Kuna haja ya kushiriki habari, utaalamu na ushirikiano wa teknolojia ikiwa tunataka mataifa yote ya kwenye jumuiya (EAC) kusonga pamoja, tunapaswa kutambua haja ya kufundisha wataalamu zaidi katika shamba, kuongeza fedha kwa ajili ya utafiti ili kuwezesha na kuboresha vumbuzi zilizopo," alisema.

Kabudi alisema uvumbuzi wa teknolojia ni chombo muhimu katika kushughulikia upungufu mbalimbali unaohusiana na sekta ya afya, zaidi ya hayo kuwekeza katika teknolojia ni kuepukika katika kujaza mapengo na kutoa ufumbuzi katika sekta ya afya.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Mohamed Kambi, akiwakilisha mapendekezo ya mkutano amesema nchi wanachama wa EAC wanatakiwa kushiriki katika maendeleo, tathmini na utaratibu wa teknolojia zinazojitokeza zinazozalishwa afya ya kidigitali na kukuza ushirikishwaji wa wafanyakazi wa afya katika kubuni vifaa vya afya ya kidigitali.

"Ushirikishwaji wa wafanyakazi wa afya katika mchakato mzima wa huduma ya afya kidigitali utahakikisha utayari kwenye kupitishwa kirahisi, kupungua kwa gharama, na kuongezeka kwa uendelevu wa huduma hiyo," alisisitiza.




Meneja Ruzuku na Mawasiliano wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald, akimkabidhi cheti John Alfred, mmoja wa washindi wa mashindano ya ubunifu ya Vodacom Hackathon yenye lengo la kutatua changamoto za elimu kiteknolojia kwa kubuni mradi wa elimu, wakati wa maonyesho ya tano ya Wiki ya Ubunifu yaliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech) hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kijaji atoa neno ujenzi wa mabweni

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ametembelea Chuo Kikuu Mzumbe na kukagua ujenzi wa mabweni ya wanafunzi unaoendelea katika eneo la Maekani, Makao Makuu ya Chuo hicho, Morogoro.

Kijaji amepongeza jitihada zilizofanywa na uongozi wa chuo kwa kushirikiana na serikali katika kutatua kero ya malazi kwa wanafunzi na kusisitiza umuhimu wa kuanza mara moja awamu ya pili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na mihadhara katika eneo hilo ili kuwarahisishia wanafunzi kutotembea umbali mrefu wakati wa masomo.

"Serikali inategemea mchango mkubwa wa vyuo vikuu katika kutimiza malengo; hasa kwenye hili la ukuaji wa uchumi. Pamoja na kwamba tunajivunia uchumi wetu kukua, lakini tusibweteke, badala yake tufanye tafiti na kuandaa vema vijana ambao watakuwa watumishi bora wa umma wanaoendana na dhana ya sasa ya nidhamu ya kazi. Hivyo, nimefarijika sana kuona maendeleo na hatua kubwa ambayo mmepiga kitaaluma na katika miradi ya maendeleo mnayosimamia," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Lughano Kusiluka, alimweleza waziri kuwa, kwa sasa Chuo Kikuu Mzumbe kinatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya miundombinu katika Kampasi Kuu ya Morogoro, Kampasi ya Mbeya na Kampasi ya Dar es Salaam na kwamba, lengo ni kuendelea kutumia ruzuku inayotolewa na serikali na vyanzo vya mapato ya ndani kuendeleza ujenzi na kuboresha miundombinu ya chuo ili kujenga mazingira bora ya utoaji wa elimu ya juu.

"Napenda kuipongeza sana serikali yetu kwa kutambua mchango mkubwa wa vyuo vikuu nchini, na kwa upande wa taaluma, chuo chetu kitaendelea kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano katika kuendeleza uchumi wa viwanda; kwa kuendelea kufanya utafiti, kubuni miradi ya maendeleo na kutoa nguvu kazi itakayowezesha Tanzania kufikia malengo yake," alisema Prof. Kusiluka.

Aliahidi Chuo Kikuu Mzumbe kuendelea kuimarisha uhusiano na kufanya kazi kwa karibu zaidi na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma kwa kubadilishana ujuzi na uzoefu, pamoja na kutumia wanataaluma kuboresha utendaji serikalini, kulinda nidhamu na kuinua kiwango cha elimu inayoendelea kutolewa na chuo hicho.

Mradi wa Ujenzi wa Mabweni katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe ambao unafadhiliwa na serikali, unatekelezwa na SUMA JKT na unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu. Mradi utagharimu Sh. bilioni 6.5 hadi utakapokamilika.

ITV
**DAKIKA 45: SAA 3:05 USIKU**
**Je, tatizo la usiri katika mikataba mbalimbali ya madini imefikia mwisho wake, na pia wawekezaji wa sekta ya madini kiasi cha faida wanayoipata kuirudisha kwenye jamii kiwango wanachotoa kweli kinastahili?. Leo Waziri wa Madini Mh. Dotto Biteko atakuwa na mtangazaji wako Deogratius Rweyunga.**

# Vodacom yaona fursa kimtandao

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya Simu za Mkononi ya Vodacom, imeanza kuwekeza katika ulimwengu wa kidijitali kwa kusaidia jamii kupitia simu za mkononi kupata huduza za kijamii.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni hiyo, Jacquiline Materu, alisema wameanzisha huduma za kidijitali ambazo wameanzisha kusaidia jamii katika afya, elimu na huduma nyinginezo.

"Kupitia taasisi yetu ya kusaidia jamii, tumeanza kufanya huduma mbalimbali ikiwamo kuwasaidia wanawake wajawazito kufahamu namna ya kujihudumia katika kipindi chote cha ujauzito hadi mtoto anapozaliwa kupitia simu zao," alisema Materu na kuongeza:

"Tumeamua pia kwenda shuleni kufundisha namna ambavyo wanafunzi wanaweza kutumia dijitali kuwanufaisha katika kujifunza mambo mbalimbali kuhusiana na elimu, na tunashukuru Mungu haya yote yanakwenda vizuri mpaka sasa huduma hii imewasaidia wengi katika maeneo hayo."

Alisema katika Wiki ya Ubunifu iliyomalizika Machi 30, mwaka huu, Vodacom wameamua kudhamini kazi mbalimbali za kibunifu kutoka kwa Watanzania ili kuhakikisha kwamba kazi zao zinatambulika na kuendelezwa.

Alisema wameamua kuwekeza katika ulimwengu wa kidijitali kwa sababu shughuli nyingi kwa sasa zinafanywa kidijitali.

Alisema lengo ni kuhakikisha Watanzania wengi wanaingia katika ulimwengu huo wa kidijitali na kuingia katika ushindani wa fursa mbalimbali zinazotumia dijitali.

"Bila kuwaandaa Watanzania sasa hivi namna ya kutumia fursa za dijitali tunaweza kubaki nyuma sana, kwa hiyo ni wakati wetu na sisi kuchangamkia fursa hii," alisema Materu.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

### KUPOTEA KWA CHETI



xxxxxxxx

**FADHILI S MUHOGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1017/0085** kilichotolewa na shule ya sekondari KIDATU mwaka 2009 ,Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .
Polisi Taarifa: **KJN/B.1/21/VOL 330**

## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga simu: 0767 223 311

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# ZIDANE AMSUBIRI RABIOT

**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya mama mzazi wa mchezaji wa Paris Saint Germain, Andrien Rabiot kukiri kuwa mwanawe yupo PSG kumalizia mkataba wake hadi mwishoni mwa msimu ili aondoke, kwa madai ya kuwa anaonekana kama mfungwa, Real Madrid imeanza kuinyatia saini ya staa huyo.

Real Madrid ambayo ipo chini ya kocha wao aliyerejea kwa awamu ya pili, Zinedine Zidane, inatajwa kuwa imeanza kumuweka katika rada zao Rabiot, huku Gazeti la AS likiripoti kwamba wameshafikia makubaliano.

Zidane ambaye amekuwa akiijaribu kuisuka upya Real Madrid ameonekana kuvutiwa na Rabiot na kwamba kuna uwezekano mkubwa akatua hapo kipindi cha majira ya joto.

Rabiot mwenye umri wa miaka 23, ameondolewa kufanya mazoezi na kikosi cha kwanza cha PSG.

Hajapata nafasi ya kuichezea PSG tangu Desemba mwaka jana, baada ya kugoma kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo.

Zidane alikuwa anataka kumsainisha Rabiot tangu msimu wa majira ya joto uliopita kabla ya kujiuzulu Real Madrid.

# Mourinho: Liverpool haitatwaa ubingwa

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jose Mourinho amesema Liverpool hawana ubavu wa kutwaa ubingwa wa Premier League kwa kuwa kuna vitu wanavikosa.

Kocha huyo Mreno ambaye hana timu kwa sasa baada ya kufukuzwa Manchester United, alihoji utimamu wa upambanaji wa Liverpool inayonolewa na Jurgen Klopp baada ya kutoka sare dhidi ya Everton, wiki moja iliyopita.

Mourinho amewataja baadhi ya wachezaji ambao anaona wameshuka ubora kwa miezi ya hivi karibuni, ambao ni James Milner na Roberto Firmino.

"Liverpool hawapo katika ubora walivyokuwa nao miezi michache iliyopita, walikuwa wakielekea pazuri. Sasa hivi Salah anakosa nafasi za wazi.

"Wiki sita zilizopita alikuwa na uwezo wa kufunga katika nafasi tofauti, lakini sasa hivi hicho hakipo.

"Milner alikuwa bora, lakini sasa hivi amekuwa hata anawekwa benchi kwa kuwa kiwango kimeshuka, ndivyo ilivyo kwa Firmino, walikuwa majeruhi na bado hawajarejea katika ubora wao," alisema kocha huyo.



# Solskjaer: Sasa nawazia ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer ameahidi kupambana kwa ajili ya kurejesha sifa ya timu yake ya Manchester United katika kupigania mataji.

Solskjaer ambaye alitangazwa kuwa kocha rasmi wa timu hiyo kwa mkataba wa miaka mitatu baada ya kuwa wa muda kwa miezi mitatu, sasa ameahidi kuwa hilo la ubingwa ndilo ambalo analifikiria.

Mkataba wake ni wa pauni milioni saba kwa mwaka, ukiwa umechagizwa na kurejesha ushindi kikosini hapo baada ya kuwa na msimu mbovu chini ya Kocha Jose Mourinho ambaye alifukuzwa Desemba, mwaka jana.

"Ubingwa wa Ligi Kuu England ndilo tunalowaza kwa sasa, kunyanyua taji ndilo jambo muhimu kwetu, tunataka kurejesha hali hiyo japokuwa siyo kazi nyepesi.

"Nataka nikiondoka niwe nimeshinda mataji, likiwamo la Premier League, ikiwa hivyo nitakuwa najivunia uwapo wangu klabuni hapa," alisema Ole na kuongeza: "Nina furaha na ni mtu ninayepambana, nataka siku nikiondoka niwe na heshima."

Wakati huohuo, United imeamua kutoa zawadi ya fedha kwa klabu ya zamani ya kocha huyo, Molde pauni 500,000 (Sh. bilioni 1.5) kama sehemu ya kushukuru kwa kumruhusu Solskjaer kuondoka.

Solskjaer pia amethibitisha kuwa msaidizi wake, Mike Phelan naye ataendelea kuwa naye klabuni hapo japokuwa atalazimika kumalizana na waajiri wake wa zamani waliomtoa kwa muda, Central Coast Mariners ya Australia.



# De Ligt: Naweza kwenda Juve

**AMSTREDAM,** Uholanzi

BEKI wa Ajax, Matthijs de Ligt amebainisha kwamba yupo tayari kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus.

De Ligt mmoja wa wachezaji wakali kwa sasa Ulaya na macho ya klabu nyingi yamekuwa yakimwangalia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, baada ya mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong kujiunga na Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi atakuwa kwenye kikosi cha Ajax kitakachoivaa Juve kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwa uhakika nampenda Giorgio Chiellini, ni mmoja wa mabeki bora duniani," alisema akiliambia Gazeti la Tuttosport.

"Pia namkubali Leonardo Bonucci, hivyo wao ni kati ya mabeki bora Ulaya.

"Naweza kujiunga na Juventus, Lakini tutaangalia katika muda mwafaka. Kwa sasa akili yangu ipo na Ajax. Wakala wangu analijua hilo."

De Ligt hana uhakika kama atakabiliana na Cristiano Ronaldo kwenye mchezo wa robo fanali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Mreno huyo kuumia misuli ya paja wakati akicheza mechi za kimataifa mapema wiki hii.



# MESSI AMKUMBUKA RONALDO LA LIGA



**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amesema kuwa anatamani mpinzani wake mkubwa, Cristiano Ronaldo angelikuwa bado yupo kwenye Ligi Kuu nchini Hispania, La Liga.

Ronaldo aliondoka Real Madrid na kujiunga na miamba ya soka nchini Italia klabu ya Juventus kwa dau la pauni milioni 100 na kuhitimisha safari yake ya miaka tisa ndani ya La Liga. Messi na Ronaldo wanaangaliwa kama moja ya wachezaji bora kabisa wa muda wote duniani na kwa sasa Muargentina huyo amesema kuwa anamkosa sana mpinzani wake Ronaldo kwenye La Liga.

"Nammisi Cristiano," alisema nyota huyo, Messi alikiambia chombo cha habari cha radio FM Club 947 nchini Argentina.

Tangu kuondoka kwa Ronaldo klabu ya Real bado haijakuwa kwenye kiwango kizuri, wakati kwenye msimamo ikiwa nafasi ya tatu ikiwa na pointi 54, huku wakitolewa kwenye hatua ya 16-bora ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushindwa kabisa kupata mbadala wa nyota huyo raia wa Ureno.


Alipotakiwa ataje mchezaji ambaye anamuona kuwa ni bora aliyewahi kukutana naye kwenye mechi alizopata kucheza nahodha huyo wa Barcelona alisema: "Sihitaji kumsahau mtu yeyote, lakini nadhani, Neymar, Kylian Mbappe, Eden Hazard, Luis Suarez na Sergio Aguero hawa ni bora sijamtaja Cristiano kwa sababu namuweka yeye kwenye nafasi yangu."

Hata hivyo, Messi amesema hayupo fiti kwa asilimia 100, zikiwa zimesalia wiki mbili kabla ya kuwavaa Manchester United kwenye robo fainali michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya CRDB na Kampuni tanzu ya Bima ya CRDB, wakionyesha medali zao baada ya kumaliza mashindano ya mbio ya CRDB Bima Marathon yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DO… ZA SOKA
## MAG…I YA ULAYA




# ZIDANE: NAPENDA SANA KUMWONA POGBA REAL

**Ninapaswa kuheshimu kwa sababu si mchezaji wangu kwa sasa, ila haimaanishi…**

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amemwelezea Paul Pogba kama "mchezaji tofauti kabisa" na kukiri kwamba angependa kuwa naye Real Madrid.

**Kiungo huyo wa Manchester United, Pogba alieleza kukunwa na Madrid wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa, akidai kuwa, kuwachezea mabingwa hao wa Ulaya chini ya Mfaransa mwenza huyo, Zidane itakuwa "ndoto" - na inaonekana kuvutiwa huko ni sawa.**

Alipoulizwa kuhusu Pogba katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mechi ya nyumbani ya La Liga dhidi ya Huesca jana, Zidane alisema: "Ninampenda sana mchezaji huyo, namjua yeye binafsi.

"Ni mchezaji tofauti kabisa, wachezaji wachache wanaweza kuchangia kile anachokifanya. Ni kiungo ambaye anajua namna gani ya kuzuia, kushambulia na kujenga mchezo. Anajua namna ya kufanya kila kitu uwanjani.

"Lakini si sehemu ya kikosi changu, yupo Manchester United, hivyo lazima tuliheshimu hilo.

"Amesema nini kuhusu Madrid na matamanio yake yajayo... kama siku moja kuna uwezekano kwamba anataka kuondoka United hivyo ni kwa nini asije Madrid."

Zidane hakuwa wazi sana wakati mshambuliaji wa Paris Saint-Germain Kylian Mbappe - mwingine aliyeripotiwa kuwindwa na Madrid - alipotajwa.

"Tunamjua mchezaji huyo, lakini si mchezaji wangu. Sitasema kwa kumheshimu, PSG, klabu yetu na wachezaji wangu," alisema.

Madrid inapitia katika wakati wa kukosa mafanikio, kwa kipindi kilichoanza chini ya uongozi wa Julen Lopetegui kabla ya kutimuliwa na kisha mikoba hiyo kupewa Santiago Solari.

Solari alidumu kwa miezi mitano tu kabla ya kurejea tena Zidane kwa awamu ya pili hapo Santiago Bernabeu.

Amerejea kwa kasi akitokea nje ya uwanja kwa kuipa Madrid pointi 12 kwenye La Liga wakati huu Barcelona ikiwa kileleni na kikosi chake kikiwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na hivyo, anatarajiwa kuwa bize mwishoni mwa msimu huu katika jiji hilo la Hispania.

"Ninatambua ni [tetesi za usajili] kwa sababu unapaswa kuzungumza kuhusu kitu fulani," alisema Zidane.

"Kuna mechi 10 zimebaki na hicho ni kitu fulani tunapaswa kufikiria, kumaliza msimu vizuri. Na si tu kwa wachezaji wangu, ambao wana mikataba, na unapaswa kuwaheshimu wale waliopo hapa.

"Pia unapaswa kuwaheshimu wachezaji ambao si wangu. Na haimaanishi kwamba baada ya hapo hapatakuwa na mabadiliko."

## ZISIKUPITE

### DAU LA ERIKSEN HILI HAPA

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, atahitaji pauni milioni 130 kutoka Real Madrid ili kumwachia kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27. ***(Mirror)***

### PSG YAMUITA DE GEA

PARIS St-Germain itafika dau la mshahara anaohitaji kipa Mhispania David de Gea, 28, pauni 350,000 kwa wiki endapo atakubali kuondoka Manchester United kwa klabu hiyo kutokuwa tayari kumlipa kiasi hicho. ***(Sun)***

### REAL, PSG, JUVE ZATUA UTD

REAL Madrid pia inapiga jaramba kwa karibu ikitaka kujiunga katika mbio moja na PSG za kumsajili kipa wa Manchester United, David De Gea, 28, wakati huu Juventus pia ikimtolea jicho. ***(Sunday Express)***

### HUDSON-ODOI KUCHUNIWA

CHELSEA haina mpango wa kuketi katika meza ya mazungumzo na winga wao, Callum Hudson-Odoi, 18, hadi majira ya joto wakati kinda huyo wa kimataifa wa England atakapokuwa amebakiza mwaka mmoja tu kumaliza mkataba wake. ***(Mail on Sunday)***

### ZIDANE AMFUNGUKIA VARANE

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesisitiza kuwa beki Raphael Varane, 25, ni mwenye furaha katika klabu hiyo licha ya kuwapo kwa tetesi zinazomhusisha na kutimkia Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### DE LIGT AKUNWA ZAIDI NA JUVE

BEKI wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, amesema anaweza kusaini kuichezea Juventus, huku kukiwa na tetesi zinazomhusisha na Liverpool na Arsenal. ***(Talksport)***

### UNITED YAITIWA RAKITIC BARCA

BARCELONA ipo tayari kusikiliza ofa ya pauni milioni 40 kwa kiungo wao Mcroatia Ivan Rakitic, 31, wakati huu Man Utd ikieleweka kuvutiwa naye. ***(Mundo Deportivo)***

### SARRI AANDALIWA MAKAO

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, ni chaguo la kwanza la Roma kuwa kocha wao kwa msimu ujao. Kocha wa zamani wa Chelsea na Leicester City, Claudio Ranieri kwa sasa ndiye anayeinoa miamba hiyo ya Serie A na ameteuliwa kushika mikoba hiyo kufuatia kutimuliwa kwa Eusebio di Francesco. ***(Sunday Express)***

### BARCA, ATLETICO KWA CHILWELL

ATLETICO Madrid na Barcelona zinamtaka beki wa kimataifa wa Leicester na England, Ben Chilwell, 22, kwa pauni milioni 50. ***(Sun)***

### WAN-BISSAKA AMULIKWA UTD

MANCHESTER United itazidi kumulika sera zake za usajili kwa wachezaji kinda, huku beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, akiwa mmoja kati ya wanaowindwa. ***(Mail on Sunday)***

### SOLSKJAER KUMVUTA ZAHA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anaweza kumfuata mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 26, ambaye alimnoa wakati akiwa Cardiff. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

# KINDOKI AMTAJA PONDAMALI USHAJAA PENALTI ALLIANCE

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BAADA ya kuisaidia timu yake kufuzu hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA, golikipa Klaus Kindoki, amefichua siri ya kiwango chake kikubwa kwenye mikwaju ya penalti dhidi Alliance FC, huku akimtaja kocha wa makipa wa timu hiyo, Juma Pondamali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kindoki alisema baada ya dakika 90 za mchezo kukamilika na matokeo kuwa bao 1-1, kocha wake, Pondamali alimfuata na kumpa maneno yaliyomtia nguvu kuelekea kwenye mikwaju ya penalti.

**"Kwanza nashukuru tumeingia hatua nyingine... kikubwa ni kujiamini tu, kocha wangu aliniambia baada ya dakika 90 kuwa nina uwezo na nikawaonyeshe watu uwezo wangu kwenye penalti," alisema Kindoki.**

Aidha, Kindoki alikiri kuwa na wakati mgumu wakati alipojiunga na timu hiyo, lakini kwa sasa amezoea mazingira ya klabu hiyo pamoja na changamoto ya mechi.

Juzi Kindoki alikuwa shujaa wa Yanga baada ya kupangua penalti ya mwisho ya Alliance na kuipeleka timu yake hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya Kombe la FA kufuatia timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90.

Kwa matokeo ya juzi, Yanga sasa itakutana na Lipuli ya Iringa kwenye hatua ya nusu fainali, ambapo mchezo huo utachezwa kwenye Uwanja wa Samora mkoani Iringa.




Daniel Manyasi akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 35.8 na balozi wa SportPesa, bondia Hassan Mwakinyo (kulia), baada ya kuibuka mshindi wa Jackpot bonasi kwa kupatia ubashiri wa mechi 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

# Muuza duka aamka na mil. 35/- SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dau la Jackpot la SportPesa kwa mshindi atakayepatia kutabiri matokeo ya mechi zote 13 kwa sasa likifikia Sh. milioni 570.3, Watanzania wanaobashiri kupitia kampuni hiyo wameendelea kujizolea mamilioni ya shilingi kila uchao kupitia bonasi maalum zinazotolewa kwa wanaopatia michezo 10, 11 na 12.

Daniel Manyasi ni mmoja wa washindi walioibuka na bonasi ya Sh. milioni 35.8 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita baada ya kupatia mechi 12 kati ya 13.

Akizungumza na SportPesa News jana, Manyasi mkazi wa Magu jijini Mwanza ameeleza safari yake ya kucheza na SportPesa, huku akifafanua kuwa kutokukata tamaa kukiwa ndio siri ya mafanikio yake.

"Nilivutiwa kucheza Jackpot ya SportPesa baada ya mshindi mmoja kukabidhiwa bajaj pale mashineni wilayani Magu, na mimi nikawa najaribu taratibu nakosea, lakini sikukata tamaa.

"Taratibu hivyo hivyo niliendelea kujaribu, mhudumu wa SportPesa akanishauri kuwa ukicheza mara nyingi zaidi ndiyo unajiongezea nafasi ya kushinda.

"Nilipoongeza mikeka mingine miwili ndiyo ukajitokeza mmoja na nikafikisha mechi 12 kati ya 13 na kuweza kupata bonasi ya Sh. 35,850,800, sikuweza kulala," alisema Manyasi ambaye ni muuzaji wa duka la rejareja baada ya kutumiwa ujumbe wa ushindi Jumapili ya Machi 24, mwaka huu.

Aliongeza: "Nilipokea meseji usiku wa saa nane, nilifurahi sana na sikuweza kulala usiku kucha mpaka sasa hivi nimekabidhiwa pesa zangu."

Licha ya kuwapo kwa kampuni zingine za kubashiri, Manyasi alifunguka kwa nini anapendelea kucheza zaidi na SportPesa.

"SportPesa wana bonasi kubwa, ndiyo maana napenda kucheza Jackpot yao na hawana longolongo, ukishinda unalipwa papo hapo.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2. Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6. Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7. TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8. Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9. Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10. Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11. Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12. Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13. JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14. Mbao | 31 | 9 | 9 | 13 | 19 | 32 | 36 |
| 15. Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16. Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17. Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19. Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20. African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

## Banana abamba bonanza mafundi

**Na Elizabeth Zaya**

MWIMBAJI wa nyimbo za Zuku, Banana Zoro, amepagawisha, katika bonanza la michezo la Kampuni ya Ufundi Zone Connect, inayohusika na masuala ya ujenzi, lililofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Katika bonanza hilo ambalo lilikuwa na lengo la kutoa burudani na kuwaleta pamoja wadau wa sekta ya ufundi ili kutoa uzoefu wao, Banana alikonga vilivyo kwa miondoko yake ya Zuku.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Jacqline Mushi, alisema lengo lingine la kuendesha bonanza hilo ni kuweka mipango na mikakati bora na kupambana na wavamizi wa sekta hiyo ambao wamekuwa wakitapeli watu.

Mushi alisema wameamua kutumia bonanza hilo kuwatambua na kuwatambulisha kwa jamii, mafundi wanaotambulika katika sekta hiyo ili kuwaepusha kutapeliwa na watu ambao wamekuwa wakitumia mafundi wasio sahihi.

"Tunaamua kufanya hivi kwa ajili ya kusaidia jamii kutambua mafundi wenye taaluma kwa sababu tayari na sekta hii nayo imevamiwa na wajanja wanaojifanya kwamba ni wajenzi kumbe ni waongo, wamekuwa wakiwatapeli watu, na tunaamini kupitia michezo tutafanikiwa kupambana na hili," alisema Jacqline huku akisisitiza Ujenzi Zone Connect wanapofanya bonanza kama hilo wanawaalika watu kwenda kukutana na mafundi sahihi.

## Shabiki Simba ashinda mil. 84/-

**Na Faustine Feliciane**

SHABIKI wa timu ya Simba, Chelsea, Juventus na Real Madrid, Semistocles Mkiza, ameshinda kiasi cha Sh. milioni 84.8 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali katika droo ya Perfect 12 inayoendeshwa na Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya M-Bet.

Mkiza ambaye ni mkazi wa Muleba mkoani Kagera aliibuka kidedea katika droo iliyofanyika Machi 24 na anakuwa mshindi nne kushinda mamilioni ya fedha kutoka kampuni hiyo kwa mwaka huu. Msemaji wa kampuni hiyo, David Malley, alisema jana kuwa wamedhihirisha kuwa wao ni nyumba ya mabingwa kutokana na kutoa mamilioni ya fedha kwa Watanzania kadhaa na kuweza kubadili maisha yao.

Malley alisema kwa kuwa kampuni yao inafuata sheria za michezo ya kubahatisha nchini, Mkiza amekatwa Sh. milioni 16. 9 kama kodi ya ushindi na kupelekwa serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kwa upande wake, Mkiza, 41, alisema kuwa amefurahi sana kushinda kiasi hicho cha fedha ambacho atakitumia kwa masuala ya maendeleo.

"Mimi ni mjasiriamari, sikuwahi kupata kiasi hiki cha fedha pamoja na kubeti mara kadhaa, nitatumia kuimarisha biashara zangu, kujenga nyuma na vile vile kusomesha watoto wangu," alisema Mkiza.

# Michezo

Jumatatu Aprili 1, 2019

Nipashe




Zidane: Napenda sana kumwona Pogba Real UKURASA 30




Beki wa kati wa Manchester United, Chris Smalling, akiwa katika harakati za kuokoa hatari dhidi ya beki wa Watford, Miguel Britos (kulia), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na United kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Bocco, Kagere vitani Simba ikiitafuta Yanga

●●● Wachana Mbao kirahisi, huku wakimtafuta Aiyee katika mbio za Kiatu baada ya kufikisha...

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

SIMBA imeendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaoushikilia baada ya kufanikiwa kuifunga Mbao FC kutoka jijini Mwanza kwa mabao 3-0 katika mchezo uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa, huku vita ya kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora ikizidi kunoga wakati huu Salim Aiyee wa Mwadui FC akiwa kileleni kwenye orodha ya wafungaji bora hadi sasa.

**Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza Mbao FC ikiwa mwenyeji iliifunga Simba bao 1-0 na ndio mchezo pekee ambao wawakilishi hao pekee wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wamepoteza katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.**

Ushindi huo wa jana ni wa 10 mfululizo kwao na umeifanya Simba kufikisha pointi 57 wakati vinara wa ligi hiyo, Yanga wana alama 67 huku African Lyon yenye pointi 22 ndio wanaoburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 31. Bao la kwanza la mabingwa hao watetezi lilifungwa na nahodha, John Bocco kwa kichwa akiunganisha mpira wa faulo uliopigwa na beki wa pembeni, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' dakika ya 24.

Nahodha huyo ambaye sasa yuko katika kiwango cha juu, alifunga bao la pili kwa njia ya penalti hilo likiwa ni la 11 kwake msimu huu, likitokana na refa kutoa adhabu hiyo kufuatia beki wa Mbao FC, Peter Mwangosi kuunawa mpira katika jitihada kuokoa hatari langoni mwao.

Dakika ya 79, Meddie Kagere alifunga bao la tatu kwa njia ya penalti baada ya yeye mwenyewe kufanyiwa faulo na Hamimu Abdullah akiwa anaelekea kufunga, hivyo sasa kufikisha mabao 14 katika msimu huu akizidiwa mawili tu na Aiyee ambaye timu yake ya Mwadui imeshashuka dimbani mara 31 mechi tisa mbele ya Simba idadi ambayo inawafanya washambuliaji wa Wekundu wa Msimbazi hao kuwa na nafasi kubwa ya kumpiku.

Katika mechi hiyo, iliyochezeshwa na mwamuzi, Charles Onoka kutoka jijini Arusha na kuhudhuriwa na mashabiki kutoka mikoa mbalimbali iliyo jirani na Morogoro, Simba ilikwenda mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0 kabla ya hayo mawili kufungwa kipindi cha pili.

Simba ilikaribia kupata bao katika dakika ya 10 katika shambulizi lililoanzia kwa Mohammad Ibrahim "Mo" kwenda kwa Bocco lakini kiungo Mnyarwanda, Haruna Niyonzima aliyekuwa ndani ya "boksi" akashindwa kumalizia na kuruhusu beki wa Mbao FC, Amos Charles kuokoa hatari hiyo. Mbao FC walijibu shambulio hilo kupitia kwa Ally Mussa, lakini Zimbwe Jr alifanikiwa kuokoa hatari hiyo baada ya mabeki wenzake kupoteana dakika ya 13.

Kagere akiwa jirani na kipa alipiga nje kwa kutumia kichwa baada ya kuunganisha krosi iliyopigwa na Niyonzima na kupoteza nafasi ya kufunga dakika ya 23.

Baada ya mechi hiyo, Kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi kitaendelea kubaki mkoani hapa kwa ajili ya kusubiri kuwakaribisha JKT Tanzania katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa keshokutwa Jumatano katika dimba hili la Jamhuri.

# Zahera: Hesabu kwa Lipuli shida

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amenusa harufu ya kukabiliana na upinzani mkali kutoka kwa wababe wao, Lipuli FC watakapokutana kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA, na sasa amepanga kuiwekea mikakati mizito ili kuweza kuibuka na ushindi dhidi ya wababe hao wa Iringa.

Yanga juzi walifanikiwa kuwatupa nje Alliance FC kwenye mchezo wa hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kwa mikwaju ya penalti 4-3 baada ya kumaliza dakika 90 kwa sare ya bao 1-1. Pamoja na ushindi huo, Zahera amewekа wazi kuwa hakufurahishwa na kiwango cha timu yake kwenye mchezo huo na kuwasifia Alliance kwamba walikuwa bora zaidi yao.

"Bado tuna kazi kubwa mbele yetu..., tuna mchezo dhidi ya Lipuli kwenye mashindano haya. Lipuli wamekuwa wakitusumbua na mchezo wa mwisho walitufunga, hivyo lazima tujipange vizuri kabla ya kuwakabili," alisema Zahera na kuongeza:

"Kwa mchezo tuliocheza na Alliance tuna kazi kubwa kuvuka, ni lazima wachezaji wangu wabadilike na kila mmoja kutimiza majukumu yake angalau kwa asilimia 90," alisema.

Aidha, alisema baadhi ya wachezaji wake hawakuwa kwenye ubora wao katika mchezo dhidi ya Alliance, hivyo kusababisha wapinzani wao hao kuwatawala.

"Kama Alliance wangekuwa makini kwenye umaliziaji walikuwa na nafasi ya kututupa nje ya mashindano..., walikuwa wazuri katikati na walikuwa na kasi kila walipokuwa na mpira," alisema.

Akiizungumzia zaidi Lipuli, Zahera aliweka wazi kuwa bado anakumbuka namna ilivyowasumbua kwenye mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa Machi 16, mwaka huu, ambapo Wanajangwani hao walilala kwa bao 1-0 na kwamba watajipanga kabla ya mchezo huo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >